

WAEBRANIA, MLANGO WA TATU



Habari za asubuhi, wapendwa. Ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo katika utumishi wa Bwana. Nasi tunatarajia na kutumainia kuwa na wakati mzuri sana.

² Nilikuwa ndiyo tu nimerudi kwenye ninii...kile tulichokuwa tukiita ofisi ya shemasi, ambamo sasa mna vinasasauti, na nilikuwa nikizungumza tu na binti mmoja na mama yake kule nyuma, wanaotoka huko juu Joliet, Illinois. Nami nilikuwa nikiwazia tu jinsi msichana huyo alivyo kazi ya neema ya Mungu. Wengi wetu tunaishi hapa tunamjua. Yeye ni m—mlevi sugu, mmoja wa aina ile walio wabaya zaidi. Wala sijapata kusikia hadithi hiyo waziwazi hadi asubuhi ya leo, jinsi ilivyokuwa wakati alipoondoka jukwaani. Bwana alikuwa amemfunulia shida zake zote na yale ambayo yangetukia. Ndipo aliondoka jukwaani, akilia na kushangilia kwa sababu Mungu alikuwa amemwokoa na ka—kaburi la mlevi. Ndipo yeye... Bibi fulani alimwendea na kuanza kulia, ya kwamba binti yake, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, alikuwa ni mtumwa wa madawa ya kulevya. Nawe unajua, kwa neema ya Mungu, msichana huyo alitwa. Ninaamini, ilikuwa ni kesho yake usiku, Rosella alitwa. Na msichana huyo wa madawa ya kulevya aliponywa. Naye pamoja na mumewe wanahubiri Injili. Na—na—na kumwona maskini msichana mzuri wa kupendeza kama Rosella, na amekolea chumvi. Na sasa yeye, anaheshimika sana, ana ninii... anasikia wito moyoni mwake. Lakini, akijua Biblia kuhusu wahubiri wanawake, unaona, anajua ni kitu kingine. Na Mungu anamwongoza kwenda kwenye magereza na kadhalika, kutoa ushuhuda.

³ Ni ajabu kabisa ku—ku—kujua, kutafuta mapenzi ya Mungu. Mara nyingine tuna hisia, bali tunataka kuchukua hisia hiyo mahali hadi mahali; usipokuwa mwangalifu, Ibilisi atachukua hisia hiyo na kuipotosha akaifanya kitu fulani. Bali almuradi tu tunadumu katika Biblia, basi tuko sahihi, unaona, tunatembea sawa na mapenzi ya Bwana.

⁴ Na kwa hiyo ninaamini ya kwamba—ya kwamba Rosella hatimaye atageukia kwenye huduma ya umishenari mahali fulani, kwa kuwa Marekani haitaki Injili.

Mnajua jambo hilo. Ni afadhali kabisa tulikubali jambo hilo, ya kwamba, hawa Waanglo-Sakson, wamekwisha. Mambo ndiyo hayo. Hakuna Injili nyingine tena ambayo Wamarekani watapokea. Loo, unapata wachache hapa na pale, mara kwa mara. Lakini, kuhusu swala la Injili, ni kwamba imekwisha. Wala hata huwezi kuwahubiria, huwezi kuzungumza nao.

Hawataamini chochote. Unaona? Wana mawazo yao ya kichwa kigumu tu, nao wamedhamiria.

Na mambo yanayofuata kwa taifa hili ni hukumu. Litaipata, hasa. Huenda ikawa ni kwa kuzorota kwa uchumi. Huenda ikawa ni kwa bomu la atomiki. Huenda ikawa ni kwa tauni kubwa, ugonjwa fulani ama kitu fulani, lakini, iko tayari. Inakuja. Maelfu mara maelfu wataangamia.

⁵ Tulipitia, jana, mimi na Ndugu Zabel, kwenye. . . na Ndugu Woods, tukirudi kutoka huko Kentucky, ambako tulikuwa kwa muda wa siku tatu, na tulipitia kwenye mradi wa kujenga nyumba. Ndugu Zabel akasema, “Hakuna. . .” Ninasahau. “Ni vigumu kumpata mmoja wa watu wale, kwenye ule mradi, ambao hata wanahudhuria kanisa lolote.”

⁶ Ungeliwauliza habari zake. “Vema! tuna televisheni yetu. Hivyo ndivyo tunavyopata faraja yetu.” Unaona? Huo ndio msimamo wa Wamarekani. Unaona? “Tuna televisheni. Tuna fedha nyingi sana. Tuna magari mazuri, tuna makazi mazuri. Tunamhitaji Bwana wa nini? Hatuhitaji jambo Hilo.” Hivyo ndivyo walivyo.

⁷ Karibu dini pekee na wokovu tulio nao, na upendo, ni mambo yaliyopo miongoni mwa wale watu halisi watauwa. Unajua, Biblia ilisema ya kwamba hayo yangetukia. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndiyo. Ninyi wasomaji wa Biblia, nimewasikia mkipaza sauti “amina,” pia na ninyi wahubiri huko nyuma. Hiyo, hiyo ni kweli. Upendo utakuwa mbali sana, katika siku za mwisho; upendo pekee ambao utasalia, ungekuwa ni kati ya Wateule wa watu wa Mungu. “Baba atamchukia mama, na mama atamchukia baba, na watoto watawachukia wazazi, na watu mbali mbali watachukiana.” Na upendo pekee utakaosalia, ungekuwa tu wa yule Mteule, Wateule peke yao. Neno “Mteule” pale linatokana na neno “Kuteuliwa,” watu wa Mungu walioteuliwa.

⁸ Na wakati Rosella alipokuwa akishuhudia hadithi hiyo kwangu mle chumbani, muda mfupi uliopita, nilikuwa tu nikiwazia, ya kwamba, usiku ule, alisema jambo fulani lilitukia. Na jinsi ambavyo alisema, maishani mwake mwote, wakati angekuwa tu mlevi sugu. Asingeweza, hakuna Shirika la Walevi Sugu. Madaktari wanne walimkatia tamaa. Hakukuwa na chochote zaidi cha kuweza kufanywa. Na jinsi, kutoka wakati uo huo, jambo fulani lilitukia.

⁹ Sasa yeye hana macho hayo ya kiwendawazimu. Yeye ni msichana mzuri sana mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, na anaokenaka kama ana miaka ishirini na miwili; jinsi tu ambavyo Mungu alimfanyia vile alivyomfanyia, na jinsi anavyoonekana wa tofauti. Na, bali nilisema, “Rosella, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Mungu aliuchagua wakati huo.” Naam, bwana. Unaona? Kweli. Na wakati maskini kijana

Billy Paul kule nyuma, pale alipo, alipokuwa akiwapa watu kadi za maombi usiku huo, jinsi ambavyo hakujua hata kidogo anampa nani kadi ya maombi.

Si ni ajabu, Rosella?

[Dada Rosella Griffin anasema, “Ndugu Branham, nataka kujua kama kanisa lingeweza kuomba ili kwamba Mungu atatuongoza, jinsi Yeye alivyokuwa mwenye nguvu.”—Mh.]

Amina. Bwana akubariki, Rosella. Nina hakika tutafanya jambo hilo. Analitaka kanisa liombe ya kwamba Mungu atamwongoza. Hiyo ni kusema, auvuate mkono Wake usiobadilika. Loo, hilo ni jambo zuri sana.

¹⁰ Nilikuwa na pendekezo la kushtusha sana nililowekewa mbele zangu, asubuhi ya leo. Ni kuhusu mtu fulani aliye milionea mara milionea anayetaka kugharimia hapa Louisville, Kentucky, na anijengee maskani ya dola milioni tano. Lakini kitu fulani ndani ya moyo wangu kilisema, “Hebu kidogo, wewe si mchungaji.” Unaona? Kwa hiyo, basi, dola milioni tano za fedha ambazo zingetengwa. Sasa kulazimika kwenda serikalini, kulipia wiski na vitu kama hivyo, bali anataka kuziweka kwenye maskani kwa ajili ya Bwana. Lakini natumaini ya kwamba zinaenda kwa mtumishi fulani wa Mungu ambaye ataninii... na utumishi fulani kwa ajili ya Mungu. Lakini, hizo ni dola milioni tano zilizotengwa sasa. Wazia jambo hilo, kwamba hizo zingejenga maskani ya namna gani.

Unaona jinsi hilo linavyoonekana la kupendeza, Rosella? Lakini kuna kitu fulani *hapa* ndani kinachosema vinginevyo. Unaona? Unaona? Kitu fulani *hapa* ndani.

¹¹ Tuliingia kwenye maskani hii ndogo, ya zamani, ninyi wageni. Vema, hapa pangeweza kuwa ni mahali pa kupendeza sana hapa pembeni, hamtambui jambo hilo, kwamba watu wametaka kupajenga mahali hapa, na kupatengeneza. Lakini hivi ndivyo jinsi tunavyopataka. Unaona, hivi ndivyo tunavyopataka. Viti vya zamani tulivyokuwa tukikalia pale, vilikuwa ni—ni vile viti vya zamani vya awali kutoka kwenye maskani hii hapa, vilivyopitia kwenye yale mafuriko vikaelea.

¹² Biblia yangu ikikaa imefunguliwa namna *hiyo* mimbarani. Iligonga kwenye dari na kurudi chini ikiwa na Neno juu Yake, “Mimi Bwana nimelipanda. Nitalitia maji mchana na usiku asije mtu akalitoa mkononi Mwangu.” Jinsi tulivyovuta makasia kupitia juu yake tukiwa na mashua ndogo, *hapa*. Nayo ikashuka kurudi moja kwa moja mahali pake, viti vikirudi moja kwa moja mahali pao. Kitu tu kilichowabidi kufanya ilikuwa ni kuisugua na kuendelea. Unaona? Unaona? Kwa hiyo hivi ndivyo tu tunavyoitaka iwe, ambapo ni ya watu wa kawaida, mahali pa kawaida, na Bwana wa ajabu. Amina.

¹³ Sasa, leo, tuna mambo fulani, tunaanza tu kuingia kwenye malai, mwajua, baada ya—ya maziwa yote kutolewa, mwisho ni

malai tu. Pia kumbukeni, inahitaji maziwa kutoa malai, mwajua. Ma—malai ni vitu vilivyomo ndani ya maziwa.

¹⁴ Kwa hiyo tumekuwa kwenye mlango wa 1, wa 2, na tunaishia kwenye wa 3, na tunaanza katika mlango wa nne wa Kitabu hiki maarufu cha Waebrania. Na, jamani, mafundisho ya Kitabu hiki! Tungeweza kudumu Nacho, kwa sababu kwenye kifungu kimoja, kwa muda wa miezi mitatu, na kuonyesha tu ya kwamba Biblia nzima inashikamana na kila kifungu katika Biblia. Je! uliwahi kuwazia jambo hilo? Hakuna hata kifungu kimoja unachoweza kuwekea kidole chako, ila kile, kwa neema na msaada wa Roho Mtakatifu, kwamba tunaweza kuunganisha Mwanzo hadi Ufunuo moja kwa moja ndani ya Hicho.

¹⁵ Hakuna kitabu kingine chochote kilichoandikwa mahali popote kinachoweza kufanya hivyo. Na kihisabati, na kijioografia, kwa kila njia, hakuna Kitabu katika Biblia kilichoandikwa kama Biblia... Hakuna kitabu ulimwenguni, ninamaanisha, kilichoandikwa kama Biblia. Hakuna chochote. Hesabu za Biblia zinapatana kikamilifu; hata tu milango, na alama za kutenga maneno, na kila kitu, ni kikamilifu. Sivyo ilivyo kwa kitabu kingine; usingeweza kusoma mlango wake mmoja bila kujipinga wenyewe. Bali hakuna kuhitilafiana hata kumoja katika Biblia nzima. Nayo iliandikwa na watu wengi, wengi, wengi; na walioachana kwa mamia, na mamia, na mamia ya miaka. Bila kujua kipande kimoja; mmoja alichandika *hapa*, na mmoja alichandika *hapa*, na mmoja alichandika *hapa*. Wakati yote ilipowekwa kwa pamoja, ilifanyiza Biblia ya Mungu. Wala hakuna hata mmoja ampingaye mwingine, na, la, wala si hisabati, jiografia zake. Kitu kingine chochote cha Biblia, kila kitu, hesabu, kila kitu kinaambatana pamoja kikamilifu. Kama huko si kuvuviwa, sijui, mtaita nini kuvuviwa? Nina furaha sana kwa ajili ya Biblia ya kale iliyobarikiwa.

¹⁶ Baadhi yao walisema, “Je! wewe ni Mkatoliki? Mprotestanti?”

Nikasema, “Si mojawapo la hayo. Ninaamini Biblia.” Hiyo ni kweli. Ninaamini Biblia, nami nina furaha ya kwamba tungali tuna uhuru wa kuihubiri katika taifa hili. Loo, ni ya ajabu sana.

¹⁷ Sasa tutaisoma toka katika Hiyo. Na sasa tutafungua katika Kitabu cha Waebrania na kuanza na mlango wa 3. Nasi tuliachia kwenye kifungu cha 15. Na sasa ninyi nyote. . .

¹⁸ Niliona mtu fulani aliona, muda mfupi uliopita, wakati nilipoichukua miwani yangu ya kusomea. Si kwamba eti macho yangu ni mabovu, bali nimepita umri wa miaka arobaini. Ninaweza kusoma, papa *hapa*, kama kawaida tu, bali ninaweza kusoma vizuri zaidi kwa miwani. Nao walinitengenezea miwani moja ya kusomea ninayotaka kutumia, kwa kuwa ninaweza kusoma vizuri zaidi na kwa haraka. Na hiyo ndiyo sababu ya kuinunua. Sasa katika ninii. . .

¹⁹ Kwanza, tunataka msingi kidogo, maana huenda kukawa na wageni miongoni mwetu, ambao hawajaipata sehemu ya kwanza ya Kitabu cha Waebrania.

²⁰ Je! wewe ni Bibi Cox, unayeketi papa hapa pembeni? Vema, kwa kweli ninafurahi kumwona, kabla tu ya kuanza, kama ushuhuda kwa neema ya Mungu. Hapa palikuwapo na mwanamke aliyekuwa na kansa ikila uso wake. Huyu ni mama yake Dada Wood. Nami nilikuwa huko Michigan pamoja na Gene na Leo, na hao wengine, wakirekodi. Na nilipokuwa nikienda zangu nyumbani, mke wangu alinipigia simu, ama nilimpigia simu. Akasema, “Ingia kwenye maombi mara moja kwa ajili ya Bibi Cox fulani, mama yake Bibi Wood, kwa kuwa kansa inaula uso wake.” Ilikuwa tayari imeingia upande mmoja wa jicho na kufikia kwenye mfupa, na moja kwa moja shavuni mwake, na inasambaa tu. Daktari fulani aliifanyia kitu fulani kingine, aliifanya kuwa mbaya zaidi, na kuitawanya tu; aliweka namna fulani ya dawa.

²¹ Nao walimleta toka huko Campbellsville, Kentucky, mpaka kwenye...ama, ninaamini, Acton, Kentucky, hadi—mpaka Louisville, akafanyiwe matibabu.

²² Na kwa hiyo Bibi Woods, ni mara ya kwanza nilipopata kumwona amefadhaika sana hivyo. Kwa sababu, bila shaka, ni mama ya—ya—yake, na bila shaka angejisikia amefadhaika. Niliingia chumbani nikamwombea, kwa ujasiri ambao Mungu alisema angejibu maombi. Na mnamo siku chache, alikuwa ametoka. Na huyo hapo sasa ameketi. Kwa neema tu ya ajabu, jinsi vile Yeye alivyomtendea.

²³ Ungeweza kusimama? Sitaki kukufanya ni—ni—ninii hadharani... Wapi, je! hiyo kansa ilikuwa iko wapi? Kwenye—kwenye upande mmoja wa shavu, unaona pale, upande *ule* wa uso wake, chini karibu na *hapa*, kufikia kwenye mfupa wa shavu lake, kwenda juu karibu na jicho lake. Na Mungu alimponya. Je! Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁴ Ni wangapi waliokuwa hapa Jumapili iliyopita kuona yale Bwana aliyofanya kwa ono? Mwanamume mmoja, kiwete na kipofu pia, akiketi papa hapa kwenye kiti cha magurudumu. Na kitu fulani kiliniumiza wakati mzee huyo aliyeketi hapa aliposema, “Ndugu Branham...” Nadhani ilikuwa ni ndugu huyu aliyepo hapa, Alisema, “Fanya vivyo hivyo kwa ajili ya mke wangu.” Yeye ana mke hapa aliye kilema. Moyo wangu uliyeyuka tu. Laiti...Ningetoa chochote ulimwenguni kama ningeweza, bali haiwezekani...sina mamlaka hayo. Bali liko katika mamlaka yangu na mamlaka yako, kuomba ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo. Yeye ana mke aliye kiwete, mkono uliopooza, na mguu uliopooza, inavyoonekana. Na mtu huyu alikuwa ana hali mbaya zaidi ya mkewe, maana huyo mke anaweza kusimama na anaweza kutembea kidogo, bali

mwanamume huyu asingeweza hata kufanya hivyo. Naye... Akili, neva kuu ya akili timamu ilikuwa imekufa. Akina Mayo, wengine wengi, walikuwa wamemkatia tamaa. Basi Mkatoliki mmoja akamwelekeza aje hapa, daktari Mkatoliki; na mvulana wake alikuwa ni kasisi huko Mt. Meinrad huko Jasper, Indiana. Lakini huko ni kuweka mawe ya msingi kwa ajili ya huo ufufuo unaokwenda, kule.

²⁵ Basi wakati aliposimama, alisema, "Lakini siwezi..." Aliangalia, akasema, "Naam, ninaweza." Alidhani asingeweza kuona, unajua. Ndipo akainua macho yake, na ikawa tu aliinua kichwa chake, na hapo aliweza kutembea na kuona; akatembea kwenye marefu hayo ya kanisa, mwenyewe. Nao walikuwa ni Wapresbiteri. Yeye alikuwa mwothodoksi. Na ninazungumza... Unafikiri ya kwamba ni Wapentekoste ama Waholiness ndio tu wanaoweza kupiga makelele; umekosea. Hakika wao wanaweza kupiga makelele wanapooona jambo kama hilo likitukia; wakikumbatiana na kupiga makelele. Akatoka moja kwa moja na kushuka kwenye vipandio, huku akisukuma kiti chake cha magurudumu; akitembea, huku neva za akili timamu zimepona. Wazia jambo hilo. Akitembea kama vile mimi na wewe tungetembea. Loo, Yeye ni wa ajabu.

²⁶ Sasa. Paulo ndiye aliyeandika Kitabu cha Waebrania. Na katika huku kuandika Waebrania, yeye ndiye aliyekiandika. Na kabla hajaandika Vitabu hivi... Tunaona sasa. Tunaenda... Hili ni darasa la shule ya Jumapili, nami nitajaribu kuangalia na wala nisichukue muda mrefu mno. Na halafu tutakuwa na ibada, tupate kuendelea nazo usiku wa leo, Bwana akipenda. Sasa, katika Kitabu cha Waebrania na Nyaraka nyingine zote za Paulo...

²⁷ Paulo alikuwa ni nani? Alikuwa ni Mwebrania hodari, msomi, na mwalimu mashuhuri wa Agano la Kale. Naye alikuwa amefundishwa na mmoja wa watu walio hodari sana wa siku zake. Mtu fulani aniambie jina lake lilikuwa ni nani. Gamalieli, mmoja wa waalimu walio maarufu sana wa siku zake. Naye Paulo alikuwa ameketi miguuni pa Gamalieli.

²⁸ Kuna kitu fulani kuhusu ninii... mahali unakoenda, kanisa gani unalohudhuria, na mwalimu gani anayekufundisha. Je! ulijua jambo hilo? Hilo, kuna jambo fulani kwake. Kwa hiyo inatupasa kutafuta yaliyo bora sana tunayoweza kupata, ili kwamba tuwe tunapata yaliyo bora sana; si kwa sababu eti ni mambo yanayopendwa na watu wengi na kadhalika, bali ni mafundisho halisi la Biblia.

²⁹ Angalia, wakati mmoja wakati Israeli walipokuwa wametoka wakaenda jangwani pamoja na majeshi yao, nao walikuwa wamepiga kambi siku saba, ndipo wakaishiwa na maji. Nao walikuwa karibu kuangamia, wakasema, "Loo, laiti kungalikuwa na nabii karibu!"

³⁰ Ndipo mmoja wao akasema, “Tuna Elisha, hapa chini. Alimimina maji kwenye mikono ya Eliya.” Unaona wenzake? Kwa maneno mengine, “Huyu hapa Elisha ambaye amekuwa na uhusiano na Eliya. Neno la Bwana liko pamoja naye.” Unalipata? Alikuwa amefundishwa vizuri. Ndipo akasema, “Yuko hapa. Hebu na tushuke twende tukamtake shauri, kwa kuwa mwalimu wake alikuwa ni Eliya, naye ana mafundisho ya Eliya ndani yake.” Unaona inaleta tofauti gani? Hakika. Tunahitaji kufundishwa.

³¹ Kwa hiyo, Paulo alipata mafundisho ya Gamalieli. Naye Gamalieli alikuwa ndiye mtu yule hodari aliyekuwa amefanya chaguo, akiwa mwanachuoni mwenyewe, ya kwamba wakati upuuzi huu wote ulipoanza wa kanisa la mwanzoni, yeye alisema, “Hebu na tusiweke mikono yetu juu ya hayo, ndugu zangu. Kama si jambo la Mungu, litashindwa, hata hivyo. Lakini kama ni la Mungu, nasi tunalipiga vita, tutajikuta tukipigana na Mungu.” Unaona, alikuwa amepata mafundisho mazuri.

³² Paulo alikuwa amekulia chini ya mtu huyu, naye alijua ya kwamba Paulo alikuwa ni mwalimu mashuhuri. Kwa hiyo, siku moja, akiwa mwaaminifu moyoni, akilitesa Kanisa, akishuka kwenda kuwakamata.

³³ Sasa hebu na tuchukue sehemu nyingine ndogo kutoka kwa Paulo, tunapopata msingi wetu.

³⁴ Wakati Yuda alipoanguka, kwa uasi, kwa kupenda fedha na kiburi cha maisha, yeye alianguka kutoka kwenye neema na akaenda mahali pake. Ndipo wanafunzi wakasema, “Hapana budi tuwe na kumi na wawili.” Ndipo kanisa, pamoja na watu wake mashuhuri, kukuonyesha vile kanisa lilivyo; pamoja na watu wake mashuhuri na nguvu zake zote, lingali limepungukiwa kwa mamilion ya maili, kwenye upeo wa ubora wake. Wakasema, “Inatupasa kumtafuta, mmoja miongoni mwetu, ambaye atapachukua mahali hapo.” Ndipo wakamchagua, kwa kupiga kura, Mathiya. Mathiasi, ninaamini, ama Mathiya. Mathiya, ninaamini ni sawa. Na wakati walipomchagua na kumweka pamoja na wale kumi na wawili, pamoja na wale kumi na mmoja, iliyofanya wawe kumi na wawili, yeye hakufanya kitu hata kimoja. Huo ndio wakati peke yake ambapo jina lake limepata kutajwa katika Maandiko. Hilo lilikuwa ni kanisa likifanya chaguo lake.

³⁵ Sasa, wao walifikiri, “Yeye ni mwungwana.” Hapana shaka. “Ni mtu mzuri sana. Ni msomi. Ana akili sana. Ni msomi. Ni mtu mzuri sana. Atapachukua mahali pa Yuda na awe mmoja wetu.”

³⁶ Lakini, unajua, Mungu wakati mwingine hufanya baadhi ya ninii. . . kwa maoni yetu, chaguzi nyingine za kijinga kabisa. Sasa, Mungu alimwona maskini Myahudi mdogo mwenye pua kama ndoana, aliyejaa hasira kama ninii, huku mdomo wake umekaa upande, “Nitashuka niende, nikawashike kila mmoja

wao. Nita—nitawatupa gerezani. Nitafanya jambo *hili*.” Hilo lilikuwa ndilo chaguo la Mungu.

Hao wengine walimchukua msomi na mwanadiplomasia. Hilo ndilo chaguo la kanisa.

³⁷ Unaona, hujui ni nani huyo aliyepo madhabahuni. Hujui huyo ni nani unayemshuhudia, gerezani ama popote pale. Huenda ikaonekana kama kwamba ni mwanandondi, maskio yake yamekunjamana, macho yake yamechunwa ngozi, na, bali wewe hujui huyo ni nani. Unajaribu bahati yako tu, hivyo tu, mpe Neno. Mungu Ndiye anayechagua.

³⁸ Basi Mungu anamchagua maskini Myahudi huyu mwenye hasira kali, ama alimchagua, hasa. Alipokuwa akienda zake barabarani, “Nitashuka niende nikawashike. Nita—nitawaonyesha hivyo ninavyoweza kufanya,” na Mungu akamwangusha tu chini.

Mungu akasema, “Hilo ndilo chaguo Langu, papo hapo.”

³⁹ Je! hilo si lingekuwa ni jambo la kipumbavu, kwa kanisa? “Mbona, yeye analitesa kanisa. Ni mtu wa mwilini.” Lakini Mungu alijua kilichokuwa ndani ya mwanadamu. Unaona ninalomaanisha?

⁴⁰ Kwa hiyo, Paulo alipata tukio. Ni wangapi wanaoamini tukio hutokana na wongofu? Hakika. Kama halikufanyika, ningetilia shaka wongofu huo. Wongofu huleta tukio. Wala huwezi kulipangia kwenye kitu chochote sasa. Mara nyingine huenda ikawa ni kupiga makelele. Mara nyingine huenda ikawa ni kunena kwa lugha. Mara nyingine huenda ikawa ni kulia kwa furaha. Mara nyingine huenda ikawa ni kuugua. Hujui ni tukio gani, kwa hiyo usijaribu kulipangia. Kwa sababu, kila mmoja wenu amethibitika kwamba amekosea katika jambo hilo, ninyi Wamethodisti, nanyi Wabaptisti, ninyi Wanazarayo, na Wapentekoste.

⁴¹ Nimeona watu wakipaaza sauti kwa nguvu sana walivyoweza kupaaaza sauti, na wakuibie dhahabu kwenye meno yako, kama wangeweza. Naam, bwana. Nimewaona watu wakinena kwa lugha kama kumwaga mbaazi juu ya ngozi kavu ya ng’ombe, na—na kwa kweli, wana kipande cha tumbaku upande mwingine wa kinywa, na wakate koo lako kama wanaligeza kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo mambo hayo hayajaninii. . . Hakuna thibitisho kwamba unaweza kuthibitisha jambo hilo, ni kwa maisha tu mtu huyo anayoishi. “Kwa matunda yao, mtawatambua.”

⁴² Kwa hiyo, hayo yote ni juu ya Mungu. Yeye huchagua. Anayakusanya mambo hayo pamoja, na hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo kama maisha yako yanalingana na matunda ya Biblia, una wazo zuri la kweli. Kama roho yako inashuhudia pamoja na Roho Yake, ya kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu, mnainii. . . Ingawa, maovu yameondoka, na kila kitu kimekuwa

kipyaa, na unaishi katika upendo, na una amani, na neema, na kadhalika, basi unakaribia sana ule Ufalme. Kwa kuwa, Uzima ulio ndani yako unatoa maisha ya aina hiyo. Unaona?

⁴³ Kama ukisema, “Loo, haleluya, nilinena kwa lugha. Haleluya!” Hilo halina maana yoyote. Hilo halina maana zaidi ya vile ungetoka uende hapa nje na kupiga wimbo kwenye gita ama chochote kile. Hilo halimaanishi kitu. Ujaponena kwa lugha, ujaopiga makelele, na kukimbia huku na huko kwenye marefu ya kanisa, na kulia machozi kana kwamba umekuwa ukimenya vitunguu, hilo halimaanishi chochote, hata kidogo, mpaka hayo maisha ya kila siku yaunge mkono barabara, yadumu na Hilo.

⁴⁴ Sasa, kama ukifanya mambo hayo, pamoja na maisha hayo, “amina,” hilo, hilo ni sawa. Hilo ni zuri. Bali unaweza kufanya mambo hayo pasipokuwa na maisha hayo.

⁴⁵ Kwa hiyo basi, si suala la kupaa sauti kwa nguvu, wala hakuna kitu kama hicho ambacho ndicho thibitisho. Yesu alisema, “Kwa matunda yao, mtawatambua.” Na tunda la Roho si kunena kwa lugha. Hilo si tunda la Roho. Kupaa sauti kwa nguvu si tunda la Roho. Kulia si tunda hili la Roho. Bali, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, utu wema, imani, upole, kiasi, hayo ndiyo matunda ya Roho. Unaona? Hayo ndiyo matunda ya Roho. Vema.

⁴⁶ Sasa, sababu ya sisi kuwa na mambo haya, watu wanapenda kuunda madhehebu, unaona. “Vema, tutayaunda. Mungu atukuzwe, wote wanaoamini jinsi *sisi* tunavyoamini, tutaelekea *huku*. Wote wanaoamini jinsi *sisi* tunavyoamini, tutaelekea *huku*.” Lakini Mungu anawataka nyote mwelekee *Huku*, kwenda juu moja kwa moja.

⁴⁷ Sasa, Paulo, baada ya kupata tukio hili, basi aliwazia kwamba hilo lilikuwa ni tukio zuri sana. Sasa, jinsi. . . Hebu—hebu—hebu na tunukuu tukio hilo kidogo. Paulo alikuwa akienda zake Dameski, kuwashika watu fulani kule chini, maana Injili ilikuwa imeshasambazwa kule. *Injili* maana yake ni “habari njema.” Na kwa hiyo walitawanyika kule, na watu wengi walikuwa wakinuka, wamejaa upendo, na furaha, na wanampenda Bwana Yesu. Na ilikuwa imesambazwa kule. Kwa hiyo, Paulo akachukua barua kutoka kwa Kuhani Mkuu. Akasema, “Nitashuka niende kule, nami nitawakamata, kila mmoja.”

⁴⁸ Kwa hiyo akachukua kundi dogo la walinzi, walinzi wa hekalu, askari, huyoo akashuka akaenda zake mbali barabarani mwendo mrefu. Walipokuwa wakienda barabarani, naye akijua yote anayoenda kufanya, mara, jambo fulani lilitukia. Mara, Nuru kuu ikatokea mbele zake. Nuru kuu, sasa, iliwaka kama jua. Hilo ni jambo la kushangaza kutukia. Nuru hiyo ilimulika hivi kwamba yeye alininii tu. . . Macho yake karibu

yapofuke. Ndipo akaanguka chini. Naye ame—amelala chini, ndipo akaangalia juu.

⁴⁹ Labda kulikuwako na watu kumi ama kumi na watano pamoja naye. Je! kuna mtu yeyote wa watu hao aliyeiona hiyo Nuru? La, bwana. Paulo aliiona. Haikukusudiwa kwao watu hao kuiona. Kwa hiyo, watu fulani wanaweza kuona mambo, ambapo, wengine hawaoni. Unaona? Kwa hiyo, Paulo aliiona hiyo Nuru, kwa kiasi kwamba hata ilimpofusha. Asingeweza kuona, kwa siku kadhaa, Hiyo ilikuwa ni dhahiri sana kwake. Wala asingeweza kuona kwa ninii kadhaa. . .

Baadaye, alipoandika nyaraka, macho yake yalimsumbua sana kutokana na hiyo, hata akaandika kwa herufi kubwa. Alisema, “Kwa kuwa nimewaandikia kwa herufi kubwa.” Aliona kwa shida.

⁵⁰ Alikuwa gerezani, naye akamsihi Bwana amponye na hilo. Naye alimsihi mara tatu. Lakini Bwana alisema nini? “Neema Yangu inatosha, Paulo.”

⁵¹ Paulo akasema, “Basi nitajitukuza katika udhaifu wangu.” Kwa maana, alisema, “Nisije nikajitukuza juu ya wingi wa Ufunuo, nilipewa mjumbe wa Ibilisi, mwiba mwilini, unaonisumbua.” Angepata nafuu kidogo, kisha yanaanza tena.

Kusumbua mana yake ni “pigo baada ya pigo.” Kama chombo baharini, unajua, mawimbi hukipiga, unaona, pigo baada ya pigo.

Naye angeninii, angepata nafuu, na kisha yamsumbue tena; kisha anapata nafuu, yanamsumbua tena. Akasema, “Bwana, kuna nini, mbona huniondolei kitu hiki?”

⁵² Akasema, “Neema yangu inatosha, Paulo. Endelea tu.” Ingedumu. . .

⁵³ Akasema, “Sasa, kama—kama ningalikuwa tu mkamilifu, na kila kitu ni kikamilifu,” kasema, “basi niliposonga mbele na maisha, loo, ningejivuna na kusema, ‘Mnaona, sina shida yoyote. Bwana ananitunza, ndugu. Haleluya!’” Hapa sasa unakuwa mwenye kujihesabia haki.

⁵⁴ Mungu hana budi kukupa kitu fulani kidogo, mara moja moja, ili kwa namna fulani akunyonyekezze kidogo, wajua. Hiyo ni kweli. Kwa namna fulani kukufanya utambue ya kwamba Yeye Ndiye Bosi. Loo, Yeye si ni wa ajabu? Naam, bwana, utukufu tu!

⁵⁵ Kwa hiyo yeye, Paulo, basi, mara baada ya kuwa na tukio hili kuu. . .

⁵⁶ Sasa, kama huyo angalikuwa ni mtu fulani siku hizi, wao wangesema, “Loo, Mungu atukuzwe, haleluya. Jamani, Bwana amenifanyia jambo fulani! Utukufu kwa Mungu!” Lakini si Paulo; yeye alikuwa ni msomi wa Biblia.

⁵⁷ Ujuzi huo hauna budi kulingana na Neno la Mungu. Naam, bwana. Kama hauambatani kabisa na Biblia... Si kuangalia tu *hapa*, useme, “Loo, ndio, hili papa hapa kabisa. Mungu ahimidiwe, nimelipata.” Naam. Hivyo sivyo Mungu anavyolitoa.

⁵⁸ Halina budi kuwa ni Biblia nzima, yote. Maana, unaweza... Makafiri wanatumia Biblia hii kama msingi wao wa kubishania. Lakini watachukua Andiko dogo *hapa*, wapindue hapa na kupata lingine dogo *hapa*, kujaribu kuyafanya yaungane pamoja, ambapo ni vitu viwili mbalimbali, kabisa. Kwa hiyo, huna budi kulifanya Andiko lilingane na Andiko.

⁵⁹ Kama Isaya alivyosema, mlango wa 28, “Haina budi kuwa ni kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, hapa kidogo, pale kidogo.” “Shikilia sana yaliyo mema.” Unaona, hivyo ndivyo jinsi linavyokuja; kanuni juu ya kanuni juu ya kanuni, Neno juu ya Neno, Andiko juu ya Andiko. Yote hayana budi kuungana pamoja. Hiyo ndiyo sababu, nafikiri, katika masomo haya kama tuliyo nayo sasa, ni jambo kuu kwa kanisa, kwa sababu linawafikisha mahali ambapo Maandiko yote yanaungana pamoja. Na tukio letu linapaswa kukabiliana na Maandiko hayo. Loo, hili hapa! Kama halikubaliani, basi ni la uongo.

⁶⁰ Na jinsi ambavyo nilitembea kwa miaka kadhaa, bila kujua hiyo Nuru iliyomwangusha Paulo chini ilikuwa ni nini. Wakati, watu huko nje, Maandiko... Hao watu, wahubiri walijaribu kuniambia, “Hayo ni ya Ibilisi. Mbona, wewe utakuwa ni mpiga ramli. Utakuwa mwanamizimu. Usijipumbaze na kitu Hicho, Billy. Kuna jambo baya kuhusiana na kitu Hicho. Usifanye hivyo, ewe kijana. Hilo ni jambo baya. Huyu ni Ibilisi. Vema, kijana, utakuwa kijumbe kabisa. Utakuwa mwanamizimu ukifanya hivyo. Loo, hayo yote ni ya Ibilisi. Hilo—hilo si sawa.” Lakini wakati... Sikutaka kuhubiri hayo.

⁶¹ Lakini alipokuwa akienda zake Dameski, Paulo hakutaka kuhubiri jambo hilo, mpaka alipopata kujua kama lilikuwa ni la kweli ama si la kweli. Kwa hiyo anashuka anaenda huko Arabuni kwa muda wa miaka mitatu, na anasoma Maandiko. Aa! Alipotoka huko, akasema, “Sasa litikiseni mlito kwangu.”

⁶² Yeye alijua ilimbidi akabiliane na Mafarisayo. Ilimbidi akabiliane na Masadukayo. Ilimbidi aukabili ulimwengu, na watu wa Mataifa. Na kwa hiyo Paulo, Biblia hii imeandikwa, Kitabu hiki cha Waebrania, kimeandikwa kwa kusudi hilo. Yeye anawatikisa hao Waebrania, na kuchukua hilo Agano la Kale na kulionyesha hapa katika Agano Jipya. “Huyu ni Mungu,” alisema, “hili hapa kwa—kwa manabii wote na kila kitu.” Anaanzia huko nyuma mwanzoni, mlango wa kwanza tuliosoma, “Mungu ambaye kwa njia nyingi, huko nyuma zamani za kale, kwa sehemu nyingi, alinena na baba zetu kwa manabii.” Hivyo ndivyo Mungu alivyoulela ujumbe Wake, uliojaribiwa

kwa Urimu Thumimu. “Lakini katika siku hizi amesema nasi kwa Mwanawe, Kristo Yesu,” aliyejaribiwa kwa Biblia Yake. Haya basi.

⁶³ Kwa hiyo matukio haya ambayo ulimwengu unasema, “Lo, ni jambo la kiakili. Mbona, hakuna mtu. . .” Wakati Malaika huyo alipotokea, ile Nuru hapa chini mtoni, wakati nilipohubiri uamsho wangu wa kwanza hapa pembeni, tuliwabatiza watu hao wote. Ninaamini, Ndugu Fleeman, huenda ulikuwa kwenye. . . Sijui kama ulikuwa hapa wakati huo ama hukuwapo. Ni wangapi waliokuwapo hapa wakati ile—wakati ile Nuru ilipotokea kule mtoni? Je! yupo mtu yote wa hao watu wa zamani hapa? Ndiyo, baadhi yao. Wakati iliposhuka hapa chini kule mtoni.

⁶⁴ Nao wakasema, “Yalikuwa ni mazingaombwe tu.” Wengi wetu tulikuwa tumesimama, tukiitazama, nayo hii hapa ikashuka. Na ndipo miaka kadhaa baadaye, Mungu alithibitisha jambo Hilo kwa jicho la kimitambo la kamera. Ni kweli.

⁶⁵ “Vema, je! ni—ni hadithi fulani ya kutunga? Je! ni kitu ambacho—ambacho. . .” La, bwana. Tunalichukua papa hapa katika Biblia na kuwaonyesha. Ni Bwana Yesu yeye yule. Hufanya jambo lile lile. Kutenda Kwake ni kule kule. Nguvu Zake ni zile zile.

⁶⁶ Angalia, Jumapili iliyopita, hapa. Huko ng’ambo, nikiwa nimelala kitandani mwangu, sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu. Ilitoka ikasema, “Kuna mtu maskanini, naye ana mvi, ana nywele nyeusi, anaanza kupata mvi. Yeye ni kipofu, wala hawezi kutembea. Yuko kwenye kiti cha magurudumu. Mtu mwenye nywele nyeusi alimtuma aje, daktari fulani, Dk. Ackerman, mtu mwenye nywele nyeusi, Mkatoliki. Alimwelekeza mtu, aliketi moja kwa moja *pale*. Na BWANA ASEMA HIVI, akasimama, akatoka akiona kwa macho yake na kila kitu. Ni kitu gani kilichofanya hivyo? Malaika yule yule yupo hapa. Yule yule aliyemwangusha chini Paulo, njiani akienda zake Dameski, anaishi katika Kanisa lake na watu Wake siku hizi. Ni Maandiko yakilingana na Maandiko. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

Loo, tuna watu walio *vuguvugu*. Tunafikia jambo hilo, punde si punde.

⁶⁷ Loo, tuna jambo lenye kilindi mbele zetu, laiti tungaliweza tu kuliingilia, leo na usiku wa leo. Sasa limeanza kuingia kwenye maji yenye kilindi. Ambapo unaninii. . .

⁶⁸ Unajua, nilipokuwa mvulana mdogo, nilikuwa na kidimbwi kidogo huko nyuma ya mahali pale, nami ningeenda huko. Na sisi sote watoto wadogo tungeingia, uchi; wadogo, yapata umri wa miaka sita, saba. Nasi. . . Maji yana kina kiasi *hiki*. Hayakuwa chochote zaidi ya kuwa mahali pa kugaagaa nguruwe mwitu. Nami nilikuwa na sanduku la sabuni pale. Ningeonyesha

kwamba niliweza kupiga mbizi; ninashika pua yangu, na kupiga maji, nikiendelea namna *hiyo*. Na tumbo langu dogo lingepiga kwenye matope, wajua, na yangeruka tu kila upande. Nikamwambia baba yangu niliweza kuogelea.

⁶⁹ Akanichukua kwenda kule nyuma siku moja. Akasema, “Ninataka kukuona ukiogelea.” Nikaruka pale, wajua; nikavua nguo zangu, kichaka kidogo makazi ya panzi; kisha nikatelemka mbio, nikayaingia maji. Nilikuwa nikirusha, matope hayo yakiruka kila upande. Na Baba alikuwa ameketi kwenye kalvati. Aliketi pale na kuniangalia kwa dakika chache. Kasema, “Toka kwenye shimo hilo la maji, na uende ukaoge, kisha uende nyumbani.” Unaona?

⁷⁰ Vema, hivyo ni kama tu vile, baadhi yetu sisi watu tunaajiita Wakristo. Tunagaagaa matopeni. Hiyo ni kweli. Mradi tu umetiwa nanga, “Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni Mpresbiteri. Nina thibitisho; ninae.” Unagaagaa matopeni.

⁷¹ Siku moja nilikuwa na mjomba wangu. Kwa muda mrefu nilimwambia. . . Yeye alikuwa na umri wa miaka kama kumi na mitano, kumi na sita. Tulikuwa tuko mtoni. Nikasema, “Mjomba Lark, ninaweza kuogelea.” Nami nilikuwa nimeketi nyuma ya mashua, unajua, nilijisikia vizuri na salama. Alitwaa tu kasia akanisukuma nje, kwenye kama futi kumi za maji. Hapo basi mambo yalikuwa ni tofauti; kupiga maji kote, kupiga makelele kote, ulikowahi kusikia maishani mwako.

⁷² Siku moja utasukumwa nje, afadhali ujue mahali unaposimama. Naam, bwana. Kama unamjua Yeye, ni afadhali umjue sawasawa. Hiyo ni kweli.

Lakini sasa tunaingia kwenye maji yenye kilindi, maji yenye kilindi, ambapo yatakufanya ufe maji kama u—kama wewe si Mkristo mzuri, aliyenepeshwa.

⁷³ Angalia hilo Neno. Paulo, kwanza alikuta hayo. Akarejea kwenye Agano la Kale, na akaona jambo hili. Aliona hilo tukio lake, waziwazi kabisa. “Sasa kilikuwa ni kitu gani Hicho kilichoniangusha chini?”

⁷⁴ Ilikuwa ni Nuru, Nuru kubwa ikisimama pale, ikiangaza kama jua, ikisimama mbele ya uso wake. Akasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

⁷⁵ Akasema, “Bwana, Wewe u nani ninayekuudhi?”

⁷⁶ Akasema, “Mimi ni Yesu.”

⁷⁷ “Nilidhani Yeye alikuwa ni mwa—mwanadamu, aliyekuwa na mikono yenye makovu, wanayedai anatokea mikutanoni sasa, akiwa na makovu ya misumari mikononi Mwake na kichwani Mwake.” La, la; si mwili *huo*, si katika mwili *huo*. Unaona? Yeye sasa ni Nuru. Sauli. . .

78 Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu. Ninarudi kwa Mungu.”

79 Yeye alikuwa ni yule Malaika aliyewaongoza wana wa Israeli katika Nuru hii, jangwani. Alirudi kwenye Nuru hiyo hiyo. Naye Paulo aliiona, kutoka katika Agano la Kale. Yeye akasema, “Mimi ni Yesu, Malaika wa Agano.”

80 Naye akafanyika mwili, apate kutukombo. “Hakuchukua namna ya Malaika,” tunaona katika milango iliyotangulia, tunaninii...kusoma. “Yeye kamwe hakuchukua asili ya Malaika, bali alikuwa ni Mzao wa Ibrahimu,” aweze kujulikana, hivi kwamba watu waweze *kumwona* Mungu. Amina.

Sasa Yeye anasema, “Nitarudi kwenye Hiyo.”

81 Na wakati Paulo alipoiona Hiyo, akasema, “Hakika, hiyo ilikuwa Ndiye. Hiyo ilikuwa Ndiye.”

82 Petro alipatwa na tukio usiku mmoja alipokuwa akiomba. Nuru hiyo hiyo iliingia jengoni, ikafungua milango mbele zake, akatoka akaingia mitaani. Na Petro alidhani alikuwa anaota; alikuwa ametiwa mafuta sana. Hakujua kile kilichotukia. Akasema, “Je, hivi nimeamka hivi punde? Lakini niko nje huko mtaani.”

83 Ndipo akashuka kwenda kwenye nyumba ya Yohana Marko. Basi yule msichana mdogo akaufungua mlango, msichana fulani mdogo pale, alikuwa kwenye mkutano wa maombi. Mtu alikuwa akibisha mlangoni. Akafungua mlango. “Loo,” akasema, “huyu hapa Petro kabisa. Mnamwombea atoke gerezeni. Bwana amemtoa.”

84 “Loo,” wao wakamwambia, “haya endelea.”

“Ee Bwana, mfungue!”

85 “Mbona,” akasema, “yeye amesimama mlangoni, akibisha.”

Petro akaendelea tu kubisha kwa nguvu sana, “Nifungulieni.”

86 “Loo,” huyo msichana akasema, “ni Petro.” Siku hizo, wangali wanacho, kizingiti kidogo cha kuvuta. Kifuniko kidogo hapa, unakiinua kwa nyuma na kuchungulia nje, unaona. Kabla hujamruhusu mgeni wako kuingia, inakubidi kujua ni nani anayebisha mlangoni pako. Sababu, walikuwa na majambazi; kama ungalifungua mlango, wangekuua.

87 Kwa hiyo, wakafungua mlango. Akasema, “Ni Petro.”

88 Wakasema, “Loo! Loo, jamani, yeye amekufa. Huyu ni Malaika wake anayesimama pale. Unaona? Amekwishaingia katika mwili wake uliotukuzwa, wajua, ule thiofania.”

89 Kumbukeni jinsi tulivyochukua jambo Hilo, ile Almasi kubwa, jinsi ilivyoakisi hiyo Nuru, jinsi ilivyorudi kule? Ninii. . . “Maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja tayari inayongoja.”

Nao walidhani Petro alikwisha kufa tayari, mwili huu wa kale ulikuwa umeanguka, nao watauzika mnamo siku chache. “Alikuwa tayari ameingia katika malaika wake, ama ninii yake iliyotuku- . . .” Sio mwili uliotukuzwa, bali katika thiofani yake, mwili ambao tayari umeandaliwa. Mwili huo usingeweza kukupa mkono. Hauna mikono ya kupeana, namna hiyo, bali uko katika sura ya mwanadamu. “Umeshuka, nao ulikuwa ukibisha mlango.”

⁹⁰ Msichana akasema, “Hata. Ni Petro. Amesimama pale.” Petro akafungua mlango pale na akaingia ndani. Huyu hapo. Sasa, Petro alikuwa amekombolewa na Nuru hii.

⁹¹ Sasa, vile vile ambavyo lile la mwanzoni . . . ambapo Paulo, katika Kanisa la mwanzoni, aliiona hiyo Nuru ya Mungu iliyommulika Paulo, Kitu kile kile kimeshuka chini. Sasa, watu wanaweza kusema chochote, hilo halilifanyi kuwa ni kweli. Bali Mungu anapothibitisha jambo lolote, kazi Yake inalithibitisha jambo hilo. Halafu, kamera inalithibitisha. Na kila kitu ambacho sisi . . . ambacho Bwana amefanya, kimethibitishwa yakini, bila kosa ya kwamba Huyu ni Mungu, kwa Maandiko, kwa jinsi inavyotenda, kwa tukio. Bali hawatasikiliza.

⁹² Angalia hapa katika maskani hii. Sasa, kumbukeni, mnajua jambo hili. Hatutamani sana kuwa na umati wa watu. Hatuna mahali pa kuwaweka, hata hivyo. Lakini angalia. Mkutano wa aina hii, mahali ambapo tulikuwa tukikutana kwa ajili ya jambo hili, unapaswa kuivutia Miji ya Falls. Bali wamekufa. Wamekufa kabisa. Wana macho wala hawawezi kuona.

Unasema, wewe, “Kwa nini, Ndugu Branham, wasiende kwa daktari wakatibiwe macho?” Hawezi kutibu aina hiyo ya kuona.

⁹³ Yesu alisema, “Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua na siku Yangu.” Akasema, “Enyi Mafarisayo vipofu. Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, bali ishara za wakati, hamwezi kuzitambua.”

⁹⁴ Je! hilo linapita juu ya kichwa chako? Sikiliza. Angalieni ishara tunazoishi ndani yake hapa. Sasa, si baadhi ya ninii tu. . . Mimi, mwenyewe, ni mwanadamu tu, wala hata si mhubiri, wa kuzungumza habari Zake. Sina elimu, kile ulimwengu unachoita, “mhubiri.” Nasi ni watu maskini tu. Angalieni hilo jengo tulimo. Angalieni hayo makanisa makuu ya dayosisi, asubuhi ya leo. Lakini angalieni mahali Mungu alipo. Jambo ndilo hilo.

⁹⁵ Vivyo hivyo ndivyo alivyokuwa Moabu akiwa amesimama pale katika fahari yake yote na uzuri wake, bali Waisraeli walikuwa kule kwenye mahema. Lakini Mungu alikuwa yuko wapi? Kulikuwako na kundi la maskini watakatifu wanaojifingirisha kule chini, wakifanya kila kitu kibaya kilichokuwako. Lakini Balaamu, askofu wa—wao, alishindwa kuona ule Mwamba uliopigwa, yule Nyoka wa Shaba, ile Nguzo

ya Moto. Macho yake yalikuwa hayaoni. Asingeweza kuiona Hiyo. Akasema, “Wao wanaliwazia tu jambo Hilo.” Lakini Yeye alikuwa yupo pale.

⁹⁶ Mungu atukuzwe, loo, Yeye yuko hapa! Mungu yupo hapa, Naye anafanya jambo lile lile ambalo amekwishafanya. Na atafanya. Tunalinganisha Andiko kwa Andiko. Mungu kamwe hajawahi kujiwakilisha kama kitu fulani kikubwa, duniani, bali daima amekaa miongoni mwa watu wa kawaida na wanyenyekevu. Naye yupo hapa asubuhi ya leo, akifanya jambo lile lile. Maandiko yanathibitisha jambo Hilo. Kamera inalithibitisha. Sasa, Hiyo, sababu ya mimi kurejea kwenye picha hiyo, si kwa sababu mimi niko humo. Mimi—mimi ni mwenye dhambi tu, aliyeokolewa kwa neema, kama mlivyo ninyi. Lakini jambo ninalojaribu kusema, ni, ni Uwepo Wake uliopo pamoja nasi. Hilo ndilo jambo muhimu. Vema, kama Yeye angelinifanya mimi kuwa Elisha a—aliyefanyika mwili, kama usingekuwa na imani ya kuamini jambo hilo, kamwe halingekufaa.

“Alikuwa kwa walio Wake. Walio Wake hawakumpokea.”

⁹⁷ Hiyo ndiyo sababu, hapa jijini siku hizi. Mbona, ningeweza kuanzisha uamsho hapa, katika jengo fulani kubwa ama kitu fulani, usingewafanya watu wengi kuamini jambo hilo. Hawataamini kabisa. Hawawezi kuamini. Siku zao zimekwisha.

⁹⁸ Somo lili hili, asubuhi ya leo, huko Afrika, lingewaleta pengine wasiopungua elfu kumi, angaa watu elfu kumi kwa Kristo. Ama, huenda ikawa kuna mwenye dhambi mmoja anayeketi hapa asubuhi ya leo, ama kitu fulani, mtu fulani aliyerudi nyuma. Karibu wote wamesakwa na kusakwa, mpaka wamekwisha kabisa. Hivyo tu.

⁹⁹ Lakini tunalojaribu kusema, ni, Andiko hulingana na Andiko. Sasa, haijalishi ni kuu jinsi gani tukio hilo lilivyo, lisipolingana na Maandiko, ni makosa.

Zile Urimu Thumimu, haidhuru nabii huyo alikuwa ni mzuri jinsi gani, kama alinena na hizo nuru kwenye hizo Urimu Thumimu hazikuwaka, jambo hilo lilikuwa ni uongo. Hata ndoto hiyo ingalionekana ni nzuri jinsi gani, kama haikumulika kwenye Urimu Thumimu, ilikuwa ni ya uongo.

Wakati ule ukuhani ulipokoma, Mungu aliweka Biblia Yake. Paulo akasema, “Kama Malaika kutoka Mbinguni angekuja,” Wagalatia 1:8, “na angehubiri injili nyingine yoyote isipokuwa ile mliyokwisha kuhubiriwa, na alaaniwe.”

¹⁰⁰ Yule malaika kutoka Mbinguni alimwambia Yohana mfunuzi, ambaye alikuwa ni Mungu Mwenyewe, “Mimi Yesu nilimtuma malaika wangu kuthibitisha, ama kuonyesha mambo haya.” Yeye alisema, “Mtu yeyote akiongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake, na yeye vile vile ataondolewa katika Kitabu cha Uzima.” *Hiki* ndicho Kitu Chenyewe, Biblia.

¹⁰¹ Kwa hiyo, matukio haya na mambo haya ambayo tunayo yakitendeka hapa, kama yasingalithibitishwa na Neno la Mungu, yangelikuwa ni uongo; sijali ni kitu gani kingetukia, ingekuwa ni uongo. Kwa hiyo ni Kweli yakini Kimaandiko. Loo, nina furaha sana mimi ni mshiriki wa ule Mwili mkuu wa Kristo.

¹⁰² Sasa, hebu na twende sasa, tunafikia kwenye somo. Sasa, tuliishia hapa ambapo yeye alisema, “Kwa kuwa tumezungukwa sasa. . .” Samahani. Hilo, nilikuwa nikinukuu mlango wa 12. Nimekuwa nikiusoma, bali sijausoma kindani. Mimi. . .

¹⁰³ Ndugu Norman, anayekaa nyumbani kwangu kule juu, naye anajua ya kwamba ndiyo kwanza niingie jana, na hao ndugu wanajua, kule chini, ndiyo kwanza niingie. Wakati pekee niliopata wa kusoma Maandiko, ulikuwa ni wakati nilipoketi papa hapa, dakika chache zilizopita. Hiyo ni kweli. Sijifunzi, ninamngojea tu Roho Mtakatifu ayatoe jinsi anavyotaka. Anajua mahali mtu huyo a—alipo, ambaye anapaswa kulipata. Kwa hiyo kama nina jambo fulani nililoazimia niani mwangu nitakalosema, basi ni makosa. Lakini kama nikimwachia tu Yeye afanye jambo hilo, atalichukua moja kwa moja mpaka mahali ambapo ni pake. Unaona? “Msifikiri mtakayosema, kwa maana si ninyi mnaonena, ni Baba yenu anayekaa ndani yenu. Ndiye anayenena.”

¹⁰⁴ Sasa, mlango wa mwisho, mlango uliotangulia, tulisikia jambo hili, ya kwamba, “Sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii; Ambao kwanza ulihubiriwa kwetu na Bwana Yesu, na Yeye pamoja na wale waliomsikia?” Mambo yale yale aliyofanya Yesu, kuwaonyesha, mambo yayo hayo kama yale yanayotukia hapa: Malaika yule yule wa Mungu, kazi zile zile, thibitisho lile lile, kila kitu vile vile, kila kitu kilichukuana, Injili ile ile, sawasawa kabisa na Neno. “Kama hilo lilifundishwa na Bwana, kisha likathibitishwa na wanafunzi Wake ambao tumewasikia,” Paulo akiwa ni yeye yule, “sisi je! tutapataje kupona, tusipoujali wokovu mkuu namna hii?”

¹⁰⁵ Sasa, Paulo alikuwa akiwaambia hayo wasikilizaji wake wa Kiebrania. Sasa, hawakuwa na vinasasauti, siku hizi, kama tulivyo navyo hapa. Bali walikuwa na waandishi waliokuwa wameketi pale, wakiyaandika wakati Paulo alipokuwa akilihubiri.

Na hivyo ndivyo ilivyo papa hapa. Tunalipata kwa vinasasauti, na kanda hizi zinasambazwa ulimwenguni kote, unaona, kuonyesha ya kwamba ni Kweli. Dini yetu si ya bure, ni Yesu Kristo yakini aliyefufuka, jambo lile lile. Sasa haitupasi kutoujali.

¹⁰⁶ Sasa, usiondoke tu kanisani, leo, na kusema, “Vema, kwa namna fulani ninafurahia kwenda kule. Ninapenda huko kuimba, na hao watu walioko kwenye maskini kanisa hilo dogo la zamani ni waungwana sana.” Usifanye hivyo.

¹⁰⁷ Ndugu, hebu achilia moyo wako uwake moto, useme, “Hapa, sina budi kufanya kitu fulani kuhusu jambo hili. Sina budi kutoka niende nione kama ninaweza kumfanya mtu fulani aoko.”

¹⁰⁸ Wala usitoke, ukisema, “Mungu atukuzwe, msipotubu, mtaangamia.” Hapana.

Liendee kwa utu wema. “Iweni na hekima kama nyoka, na wapole kama hua.” Unaona, hivyo ndivyo mnavyopaswa kwenda. Mwendee mtu huyo, kama anafuga kuku, mzungumzie kuhusu kuku, kwa muda kidogo. Unaona? Na baadaye basi, muda si muda unajua, mtakuwa mkinena habari za Bwana. Kama yeye ni mkulima, zungumza kuhusu shamba lake.

¹⁰⁹ Kama anauza magari, zungumza juu ya magari yake, kwa muda kidogo, “Una magari mazuri kwelikweli,” na kadhalika. Unaona?

¹¹⁰ Mpaka utakapoishika hiyo Roho, wakati Baba anaposema, “Sasa huu ndio wakati wa kumkaribia kuhusu nafsi yake.”

¹¹¹ Unaweza kumalizia, unaona, “Hilo ni gari zuri. Unajua usafirishaji, siku hizi, umekuwa ni jambo muhimu. Loo, jinsi ambavyo mataifa yameletwa karibu pamoja; na majiji ya mataifa yetu, karibu pamoja. Marafiki na akina mama wanaweza kutembeleana. Unajua, ni jambo la ajabu kuwa na magari kama haya unayouza.”

¹¹² “Naam, bwana. Hakika hivyo ndivyo ilivyo. Ndio.” Unajua, akipuliza msokoto wake, ama chochote kile. “Naam, hayo, hayo ni magari mazuri.”

¹¹³ “Je! uliwahi kuwazia jinsi watu wa kale wangelifikiri kama wangeliona kitu kama hicho?” Endelea tu namna hiyo, wajua.

Punde si punde, useme, “Naam, ndio, hakika ndivyo ilivyo.”

¹¹⁴ “Unajua, jambo lingine hilo linafanya, linaleta kama sisi kuwa na ninii, kama katika miamsho. Watu wanaweza kuja kutoka kote nchini, haraka, kwa ajili ya uamsho.” Unaona, unafungua njia, wakati wote, wajua.

¹¹⁵ Kama ukisikia kitu kikiifunga njia, simama papo hapo, soge *hapa*. Kama vile daktari fulani alivyosema, huko Phoenix, alisema, “Bwana, ujaze mdomo wangu na maneno mazuri, kisha uniguse na kiwiko nikiisha kusema ya kutosha.” Unaona? Naam. “Niguse na kiwiko nikiisha kusema ya kutosha.”

¹¹⁶ Sasa, angalia sasa, tutaanzia kwenye kifungu cha 15, ama kifungu cha 15 cha mlango wa 3, kwa makini sasa.

Hapo inenwapo, Leo, kama ninyi... mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha,

¹¹⁷ Sasa mwangelie Paulo akinena hapa. Sasa inasemwa, “Leo, baada ya muda mrefu.” Tutaliingilia hilo baada ya kitambo

kidogo, ya kwamba, “Leo, muda mrefu sana.” Inakuja kwenye mlango unaofuata, “Baada ya muda mrefu.”

...inenwapo, Leo, kama ninyi...mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha, wakati walipomkasirisha Mungu.

118 Sasa hebu na tusome kifungu kinachofuata.

Kwa kuwa wengine, walipokwisha kusikia, walimkasirisha...

Sasa, yeye anazungumza juu ya nini? Injili.

...si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa?

Tena ni akina nani aliochukizwa nao kwa miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?

119 Hebu na tukomee hapa kwa dakika moja. Kule *kukasirisha*, “walipomkasirisha.” Sasa Mungu alifanya nini? Sasa Paulo anajaribu kuzungumza. Ni kitu gani kilichowaongoza kutoka Misri? Je! ilikuwa ni Musa? La. Musa alikuwa ni chombo cha mwili.

120 Sasa tuna msingi hapa. Tunataka kunyoshwa vizuri sasa. Tutakapofikia mahali hapa, katika dakika chache, mta—mtaona jambo hilo.

121 Sasa, Mungu alikuwa na watu wake waliokuwa hawajapata raha. Walikuwa huko Misri. Walikuwa wameondoka kwenye nafasi yao sahihi. Walikuwa nje ya nchi ya uenyeji wao. Walikuwa ni wageni na wasafiri, naye Mungu alikuwa anaenda kuwatoa huko walikozuliwa, huko—huko Misri, kuwapeleka hadi kwenye nchi ya uenyeji wao.

122 Mfano wa siku hizi; sisi tunahangaika. Hapa hapana muda mrefu. Maskini wavulana wenye mikono minene wakicheza marumaru, wasichana wadogo wakiwa na wanaserere, wakicheza; muda si muda wajua, una mvi, na unapata makunyanzi. Pana kasoro fulani hapa. Hapa si nyumbani. Tuko mahali pasipotupasa kuwa. Hiyo ndiyo sababu tunasema sisi ni wasafiri na wageni. Jambo fulani limetukia.

123 Maskini bibi mmoja mdogo alisema, asubuhi ya leo huko chumbani, jinsi ambavyo watu humcheka, wakati fulani. Nikasema, “Lakini, dada, mpenzi, wewe si mmoja wao.” Sisi ni watu tofauti.

124 Msichana wangu mdogo alisema, “Baba, wasichana *fulani* walifanya mambo *fulani* waliyofanya.”

125 Nikasema, “Lakini, angalia, mpenzi.” Walikuwa na sahani hizi za santuri za Elvis Presley. Nikasema, “Nisingezitaka nyumbani mwangu.”

126 Akasema, “Lakini, baba, wao ni wasichana wadogo wazuri.”

¹²⁷ Nikasema, “Huenda wakawa. Sina neno la kusema dhidi ya jambo hilo. Lakini kuna jambo moja, sisi tuko tofauti. Sisi tuko tofauti. Si eti kwamba tunataka kuwa tofauti, bali Roho aliye ndani yetu ametoka kwenye mambo hayo. Wewe ni wa ulimwengu mwingine.”

¹²⁸ Ninapoenda Afrika, siwezi kuzoea maisha yao wa—wa—wanayoishi. Hawavai nguo zozote. Wako uchi. Nao wanaokota kitu kilichooza, kina mabuu ndani yake, wanakila, hata hivyo; hakileti tofauti yoyote. Unaona?

¹²⁹ Na Hili ni tofauti. Unajua, wakati mmoja, sote tulikuwa namna hiyo, lakini ustaarabu umetuleta na kutufanya tofauti.

Nao wongofu umekuza hayo kwa milioni. Hatutaki vitu vilivyooza vya ulimwenguni tena. Kristo ametufanya kuwa Wakristo; kama vile ambavyo ustaarabu umetufanya tuwe wasafi. Pia angalia, si hayo tu, bali tunakiri ya kwamba sisi ni wasafiri na wageni. Sisi si wa ulimwengu. Basi, hutaki jambo lolote linalohusika na ulimwengu. Na mambo hayo yamepita.

¹³⁰ Sasa, Israeli walikuwa huko Misri. Hawakuwa ni Wamisri. Wamisri, ilikuwa ni fedheha kwa Mmisri kuweka mkono wake juu ya kondoo. Nao Israeli walikuwa ni wachungaji. Na jinsi ambavyo hapana budi lilimgusa Musa, baada ya aibu yote waliyopata ya kuwa Mmisri, wachunga ng’ombe.

Je! uliwahi kuona vile Farao alivyokuwa amemwambia Yusufu, na kadhalika? “Ni chukizo.” Kasema, “Watu wako ni wachungaji.” Na hata Mmisri asingeweza kuiweka mikono yake juu ya mchungaji. Alikuwa ni mtu tofauti.

¹³¹ Na hivyo ndivyo ilivyo na Mkristo, siku hizi, anapozaliwa mara ya pili. Si ninii. . .Ni uchafu kwake kushiriki mahali ambapo watu wanakunywa pombe na kufanya mizaha michafu, na wanawake wako uchi. Na kila. . .Hilo, ni—ni uchafu. Loo, Bwana na atukuzwe! Sisi ni wasafiri hapa. Sisi ni wageni hapa. Roho imekwisha kuongoka, nasi tunautazamia Mji ambako wanawake hawavai kaptura. Tunautazamia Mji ambako hawana vilabu vya pombe. Tunautazamia Mji ambamo haki inakaa. Kwa hiyo, sisi ni wasafiri.

¹³² Kwa hiyo, Mungu alishuka katika mkusanyiko mkubwa wa Moto, kama Duara ya Mwangaza, akashuka kwenye kijiti na akaanza kujifunua kwa Musa, kwanza. Musa akasema. . .

Unajua jinsi tulivyokuwa na lile somo hivi majuzi usiku, jinsi vile ambavyo Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Vema, Musa asijakuwapo, MIMI NIKO.” Yule alikuwa ni Yesu kwenye kijiti kilichowaka moto, katika Nguzo ya Moto. Ni Yesu, leo, yule yule.

Naye alijifunua Mwenyewe katika Nguzo ya Moto, ndipo Musa akapata tukio. Anashuka kwenda Misri. Anaihubiri Injili,

habari njema, na ishara na maajabu yalimfuata. Unalipata? Jambo lile lile siku hizi.

¹³³ Si hilo tu, bali hao Waebrania walitoka, wakatembea katika Nuru, waliongozwa na Nguzo ile ile ya Moto. Nayo Biblia ilisema ya kwamba, “Msimjaribu Mungu.”

¹³⁴ Angalia jambo hili. Hebu nilisome.

Hapo inenwapo, Leo, kama ninyi...mtaisikia sauti yake, msifanye migumu moyo wenu, sauti yake ikizungumza na moyo wako, kama wakati wa kukasirisha, wakati walipomkasirisha.

Sikilizeni.

Kwa kuwa wengine, baada ya kusikia, walimkasirisha...

¹³⁵ Ni wangapi wanaojua ya kwamba Waisraeli walimkasirisha Mungu kwa kutokuamini kwao? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Walinung’unika. Walininii kabisa...Mungu alishuka akaenda moja kwa moja kule. Na wakati waliponinii kabisa...Jambo la kwanza, waliingia katika shida.

Hii hapa Nguzo ya Moto juu yao. Sijui kama wote waliiona, ama hawakuiona. Angalau, Musa aliiona. Nayo ilikuwa juu yao, nao waliangalia. Na waliposhuka...Tuseme kama hawakuiona, sijui kama waliiona ama hawakuiona. Iliwatangulia. Biblia ilisema ilikuwapo pale.

¹³⁶ Ilisema, “Ile Nyota iliwatangulia wale mamajusi.” Hakuna mtu aliyeiona ila wale mamajusi. Ilipita juu ya kila kituo cha uchunguzi wa nyota. Waliangalia majira kwa nyota. Hakuna mtu aliyeiona ila wale mamajusi. Ilikusudiwa wao waione, na hao mamajusi ndio waliotumiwa hiyo Nyota.

¹³⁷ Na Nguzo ya Moto ilitumwa kwa Musa, na Musa alitumwa kwa wana wa Israeli. Nao walipaswa kumfuata Musa. Waliweza kumwona Musa, na Musa aliiona ile Nuru.

Hao hapo wakienda!...?...Nao walipokuwa wakitoka, walifika kwenye Bahari ya Shamu. Na, loo, wao—wao kamwe hawakuona ishara hizo zote za miujiza na mambo kadha wa kadha yakitukia wakati walipokuwa wangali kule chini katika—katika nchi ile ya kale ya Misri, bali walipotoka wakaenda huko nje katika safari yao, ndio tu wameongoka na kutolewa. Ndipo, muda si muda unajua, waliingia katika shida.

¹³⁸ Mungu anapenda kukuingiza katika shida. Yeye anapenda kushusha shida aone utakalofanya kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo aliweka tu kizuizi cha Bahari ya Shamu, na muda si muda unajua, akawaongoza akawaingiza mahali hapa, kisha akamfungulia Farao awafuate. Unaona jinsi Mungu anavyopenda kufanya jambo hilo? Anapenda kuonyesha nguvu Zake na upendo Wake. Yeye ni Mungu, Naye anapenda tu kukuonyesha wewe kwamba yeye ni Nani. Amina.

Na shida yake ni kwamba, siku hizi, watu husema, “Loo, siku hizo zimepita.” La. Mungu anawezaje kujionyesha, wakati unapofundishwa upuuzi kama huo? Bali Mungu anapenda kujidhihirisha Mwenyewe.

¹³⁹ Hawa hapa wana wa Israeli wakaja, wakitembea katika Nuru. Musa, akiwatangulia. Hao hapo. “Njoni. Njia ndiyo *hii*. Mungu anaita. Tunatoka. Tunaenda kwenye nchi ya ahadi.”

“Loo, haleluya!” Hawa hapa wote, wakipiga makelele, na kurukaruka, na wakiwa na wakati wa furaha, unajua. Na muda si muda unajua, waliangalia nyuma na kusema, “Loo, vumbi lile ni la nini?”

¹⁴⁰ Mmoja wao akapanda juu ya kilima, akasema, “Loo, loo! ole, ole! Ni jeshi la Farao.”

¹⁴¹ Mungu akasema, “Mnaogopa nini hivi? Hivi hamkuamini niliyotenda kule nyuma? Ni kitu gani kinawafadhaisha hivi? Kwa nini mnanikasirisha?”

¹⁴² Waliopofika kule, Musa alitoka akaenda na kumsihi Mungu. Mungu akaifungua tu Bahari ya Shamu nao wakavuka; akamfungia adui humo ndani. Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Usiogope. Usitaharuki. Usiwe na wasiwasi. Unamkasirisha Mungu.

¹⁴³ Basi Yeye alifanya nini? Inaonekana kama, “Vema, tulikuwa na jaribio moja kubwa; Mungu atukuzwe, tulivuka. Hatutakuwa na mengine. Tuko njiani kuelekea kwenye nchi ya ahadi.” Ndipo akawaongoza moja kwa moja kuingia jangwani, ambako hakuna maji. Ungeweza kuwazia? Mungu, akiwa na nanii Wake—akiwa na watu Wake waliotakaswa, watakatifu, aliwaongoza moja kwa moja akawaingiza kwenye mtego *huu*; kisha akawatoa kwenye mtego huo, na akawaongoza moja kwa moja mpaka sehemu hii mahali pasipokuwapo na maji. Ambapo angeweza kuwachukua awapitishe kwa njia nyingine ambako kungekuwa na maji. Mbona, angaliweza tu kuumba mto, utiririke njia nzima, kama angalitaka. Angaliweza kulipua kila mlima ukaleta shangwe, ukirusha maji futi hamsini hewani, kama angalitaka. Hakika, angeweza. Lakini kama angalifanya hivyo, ingekuwa ni jambo rahisi sana. Loo, jamani! Jina la Bwana litukuzwe.

¹⁴⁴ “Kwa nini Mungu aliacha jambo *hili* litukie, Ndugu Branham? Ni kwa nini Mungu alifanya hivi?”

Mungu anafanya jambo hilo. Mwache. Endelea tu kusonga mbele. Hilo ni shauri la Mungu. “Nyayo za mwenye haki zinaongozwa na Bwana.” Naam, bwana. Inaleta tofauti gani?

¹⁴⁵ “Nimepoteza fedha zangu zote, Ndugu Branham.” Vema, Mungu atukuzwe, hata hivyo.

¹⁴⁶ “Loo, nilifanya *hili*, na *hili* likatukia, dhoruba ilibomoa nyumba yangu.”

147 Mungu atukuzwe, hata hivyo. “Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana litukuzwe.” Endelea tu kusonga mbele. Yote ni utukufu wa Mungu. Mungu anajua analofanya.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia
kwenye mafuriko,

Wengine kupitia katika majaribu makali, bali
wote hupitia kwenye Damu.

148 Hivyo ndivyo anavyotuongoza. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Ninajisikia kana kwamba ningesimama tu na kupiga mayowe. Hivyo ndivyo anavyowaongoza watoto Wake wapendwa. Loo, je! unaweza tu kusikia . . . Sasa, mimi si mwanasaikolojia, bali je! mnaweza tu kuhisi Roho huyo wa kupendeza sasa akifurika kwenye jengo hili? [Kusanyiko linasema, “Amina,”—Mh.] Vipi kama macho yetu yangefunguka sasa hivi, na kuangalia kile kinachosimama karibu na pande za kuta hizi, huku na huko kwenye marefu ya kanisa?

149 Ee Elisha! Asubuhi moja, wakati mvulana huyo alipokuwa kipofu tu alivyoweza kuwa, yeye alisema, “Angalia hao Waashuri kule chini.”

Kasema, “Lakini kuna wengi zaidi walio pamoja nasi.”

Kasema, “Sioni mtu.”

Kasema, “Bwana, yafungue macho ya mvulana huyo.”

150 Aliangalia pande zote kumzunguka nabii huyo mzee, mahali pote hapo, milima ilikuwa ikiwaka Moto, na farasi wa Moto, na magari ya Moto. Ndipo basi aliporidhika.

151 Akasema, “Tutatoka twende tu na tukawapige kwa upofu.” Macho yao yalikuwa ni mazuri tu kama yalivyopata kuwa, bali walikuwa ni vipofu kwake. Kasema, “Ati ninyi nyote mnamtafuta Eliya?”

Kasema, “Naam, bwana.”

152 “Njoni, nitawaonyesha mahali aliko.” Na huyo alikuwa ndiye, akiwaongoza. Hawakujua jambo hilo.

153 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Kristo yupo hapa. Roho Mtakatifu yupo hapa, akifanya mambo yale yale ambayo amekuwa akifanya daima, nao ulimwengu ni kipofu kwa Hayo. Hawajui jambo Hilo. “Loo, si—sijui kuhusu jambo Hilo. Mchungaji wangu. . .” Loo, enyi maskini watu dhaifu! Mnaona ninalomaanisha? Ni vipofu kwa Hilo. Hawajui jambo Hilo. Mungu anaongoza.

154 Sasa, walipanda wakaja, kupitia kwenye Bara ya Sini, hakukuwako na maji kule. Mungu alikuwa ameandaa kila kitu. Loo, ndipo wakakuta kidimbwi cha maji, wakasema, “Haya hapa maji.” Wala wasingeweza hata kuyaonja. Loo, yalikuwa mabaya sana. Jamani, ni—ni mabaya kuliko asilimia mia moja ya salfa. Unaona, ni kama tu mayai yaliyooza, unajua. “Loo,

jamani! Ni mabaya sana.”Yalikuwa ni sumu. Sasa, iliitwa Bara ya Sini. Mitende kadhaa hukua pale, na chemchemi ambapo mitende hiyo ilikua. Ndipo Musa akasema, “Msininii. . .”

¹⁵⁵ Mungu akasema, “Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini wananikasirisha? Vema, kama nilifanya vile *kule* nyuma, hivi siwezi kufanya jambo fulani kuhusu hali hii?”

¹⁵⁶ Kama alikutoa kutoka katika janga moja, hivi hawezi kukutoa kwenye jingine? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Alikutoa kutoka katika shida moja, hivi hawezi kukutoa kutoka katika nyingine? [“Amina.”] Mungu atukuzwe! Kama alinitoa kutoka katika dhambi, anaweza kunitoa kutoka kaburini. Yeye ni Mungu. Inaleta tofauti gani? Endelea tu, endelea kumtazama Yeye.

¹⁵⁷ Kasema, “Kama nilifunga Bahari ya Shamu nyuma, na kuwazamisha majini hao Wamisri, hivi siwezi kufanya jambo fulani kuhusu maji haya? Kwa nini mnanikasirisha? Loo, kutokuamini kwenu! Mnanikasirisha, kwa sababu ya kutokuamini.”

¹⁵⁸ Sasa neno hapa linalotumika ni, “Dhambi,” kukasirisha. Walifanya. . .Sababu ya kufanya hivyo, hawakuamini. Hawakutoka wakaanza kucheza dadu, sasa, na vitu kama hivyo. Hawakutoka na kwenda kufanya yasiyofaa na mke wa mtu fulani, na wakatoka wakaenda kusema uongo. Hivyo sivyo walivyokuwa wakifanya. Lakini, hiyo si dhambi, kwanza.

¹⁵⁹ Kuishi katika uzinzi si dhambi. Kuvuta sigara, kutafuna tumbaku, kunywa pombe, kucheza kamari, kulaani, kuapa, na kadhalika, hayo si dhambi. Hayo ni matokea ya kutokuamini. Unafanya hayo kwa kuwa wewe ni asiyeamini. Kama wewe ni mwamini, hufanyi mambo hayo. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na *kumwamini* Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Si *asemaye* anaamini, bali anayeamini hasa! Hilo hapo. Hilo linaondolea mbali thibitisho lenu la kwanza lote. Unaona? Sasa, haya basi.

Si, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kupaaaza sauti.” Si, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kunena kwa lugha.” Si, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na ana damu mkononi mwake ama usoni mwake,” ama chochote kile tena. Sio Hilo.

“Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na *kumwamini* Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia kamwe Hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani.”

¹⁶⁰ Dhambi ni kitu gani? Kutokuamini. Kitu fulani kidogo kinaweza kikainuka, badala ya kwenda moja kwa moja kwenye Maandiko na kuona kama ni kweli ama si kweli, “Loo,” unasema, “Mimi ni ninii. . .” Saa! Unaona, hapo, endelea tu. “Nitaendelea tu kuwa Mpresbiteri kama nilivyo, unaona.” Endelea, ewe kipofu, nawe unamkasirisha Mungu.

161 Mungu anapofanya jambo lolote, analitarajia taifa kulishika haraka. Lakini, badala ya kulishika, “Unajua, vema, sijui kuhusu jambo Hilo.” Unaona? Yeye anawatarajia watu kulipata. Kama unahusika vya kutosha, keti chini na Maandiko. Yapitie na uyachunguze, mbele na nyuma, na uone kama jambo Hilo lilitukia, kama limetabiriwa kuja kutimia, na kadhalika. Ndipo utalipata. Amina.

162 Sasa angalia.

Hapo . . . Leo, kama ninyi . . . mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha, wakati Mungu alipokasirishwa nao, unaona.

Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia? Waliposikia injili aliyohubiri Musa, walimkasirisha: si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa?

163 Ni wangapi wanajua ni watu wangapi waliokolewa kutoka katika kundi hilo la mwanzo lililotoka? Ni wangapi? [Mtu fulani anasema, “Wawili.”—Mh.] Wawili, ni sawa. Ni wangapi wanaojua majina yao? [“Kalebu na Yoshua.”] Hilo ni sawa. Kalebu na Yoshua, hao wawili peke yao, kutoka katika milioni mbili na kitu.

164 Sikilizeni hili. “Lakini yeye. . .” Kifungu cha 17 sasa.

Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini, kwa ajili ya kutokuamini. Si wale waliokosa, wasioamini. . . ?

165 Chukua kamusi uone *dhambi* maana yake ni nini. Chukua kamusi ya Biblia. Ni kutokuamini. *Kutokuamini* ni “dhambi.” “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa,” Yohana Mtakatifu 4, unaona, “amekwisha kuhukumiwa.”

. . . ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?

Tena ni akina nani aliowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake, . . .

166 Kutokuamini kwako! Loo, jinsi ambavyo sitaweza kamwe kuufikia mlango wangu. Lakini, angalia, hiyo ndiyo shida ya taifa hili, siku hizi. Ishara na maajabu yamepita humu nchini. Watu wanafanya nini? Daima wanalipa jambo hilo kisogo. Naye akasema, “Nitaapa ya kwamba sitawaruhusu kuingia katika Nchi waliyoelekea kwenda.”

167 Kuna shida gani na makanisa haya makubwa siku hizi? Kutokuamini kwao kumemkasirisha Mungu. Haleluya! Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Yeye alijaribu kuwapa Injili, nao wakaifanya migumu mioyo yao. Wanajiundia vikundi, kisha wakafanya madhehebu madogo madogo, “Nasi tunaamini *hivi* wala hakuna kitu kingine,” wala Mungu asingeweza kuingia ndani. Wako wapi siku hizi? Wameketi kando ya njia.

¹⁶⁸ Kundi dogo la Mungu lililo aminifu, linasonga mbele moja kwa moja, pamoja na ishara na maajabu. Yeye anawapa majaribio. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kwanza kujaribiwa na kuchunguzwa,” mtoto aliyefunzwa.

¹⁶⁹ Jambo dogo la kwanza lilipotukia, “Loo, vema, labda hakuna kitu chochote kwenye jambo Hilo, hata hivyo.” Wewe ndiye yule mtoto haramu, wala si mwana wa Mungu.

¹⁷⁰ Kwa kuwa mwana wa Mungu ni Mzao wa Ibrahimu, ambaye anayaita mambo yale ambayo hayakuwako, kana kwamba yalikuwako, “Mungu alisema hivyo,” na anaendelea tu kusonga mbele. Amina. Haidhuru ni kitu gani kinachosemwa, ama chochote kingine, wanaendelea kusonga mbele, hata hivyo. “Mungu alisema hivyo.”

¹⁷¹ Alimngojea mtoto huyo kwa muda wa miaka ishirini na mitano, haidhuru lilikuwa ni jambo la kinyume jinsi gani. Naye alijitenga na hao wasioamini, amina, kusudi apate kuamini. Loo, jamani! Ninajisikia wa kiroho.

Wazia jambo hilo. Inakupasa kujitenga na hilo fundisho la sharti la ulimwengu, “Aa, hizo siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Hicho. Hizo ni siasa kali.” Jitenge nao.

¹⁷² Biblia ilisema, “Tokeni kwao, mkatengwe nao, asema Bwana, nami nitawapokea.” Ni ajabu jinsi gani! “Nitawapokea, baada ya ninyi kujitenga. Mtakuwa watoto wangu. Nitakuwa Mungu wenu. Jitengeni. Msijifungie nira pamoja na wasioamini.” Hiyo ni kweli.

¹⁷³ Kijana mwanamume anayetaka kuo, alimwoa msichana asiyeamini; ama msichana mbichi anaolewa na mvulana asiyeamini. Usifanye hivyo. Sijali huyo mvulana ana sura nzuri vipi, na—na, ama huyo msichana ni mzuri jinsi gani, na vile macho hayo makubwa aliyo nayo yalivyo; yote yatafifia moja ya siku hizi. Lakini, ndugu, nafsi yako itaishi milele. Uwe mwangalifu kwa yale unayofanya. Kama huyo msichana si mwaminio halisi, ama huyo mvulana si mwaminio halisi, usijifungie nira namna hiyo. Kaa mbali na hilo. Yatakuletea shida safarini.

¹⁷⁴ Sasa sikilizeni, kifungu cha 17.

Tena...nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?

...ni akina nani aliowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake,...

¹⁷⁵ Walianza kutoka, bali waliona miujiza, bali kamwe hawakuingia katika nchi ya ahadi. Ni wachache tu waliochaguliwa, wawili wao, walioingia kwenye nchi ya ahadi.

¹⁷⁶ Sasa Paulo anafanya nini? Anawazungumzia Wakristo sasa, “Msiache Injili ii hii, iliyohubiriwa kule nyuma, katika ishara

na maajabu, na Nguzo ya Moto ikawaongoza; wakati mambo haya yatakapoanza kutukia tena, msiangukie kando ya njia, kwa kutokuamini, mwanze kutilia shaka, kwa kuwa mizoga yao ilianguka nyikani.”

177 Sasa tunaingia, upesi sasa. Angalia kwa makini.

...ila wale wasioishi?

Basi twaona ya hawapaswi kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao.

Yeye anaita hilo ni *dhambi* hapo nyuma, anaita hilo *kutokuamini* wakati mwingine. *Kutokuamini* ni “dhambi.” “Hawakuingia, kwa sababu ya kutokuamini kwao.”

178 Walimwona nabii huyo, Musa. Waliona yale aliyofanya, wakaona yale aliyosema. Yalikuwa ni kweli, kila wakati, wakasonga mbele moja kwa moja kwenye Ukweli. Nguzo hii ya Moto ingetokea mbele zao. Waliitazama. Waliiona.

179 Paulo, akijaribu kupata, baadaye kidogo, kuangalia hapa kwa ndani, lile tukio alilokuwa nalo. Unaona? Akijaribu kusimulia tukio hilo, alilifananisha na Agano la Kale. Alisema, “Sasa tumeingia katika jambo jipya, kwenye kipindi hiki kipya cha wakati, kwa Yesu Kristo. Zamani za kale, Bwana aliwatokea katika manabii, lakini sasa anawatokea katika Mwanawe, Yesu.” Unaona? Naye anaingia ndani, kufananisha matukio hayo na kuwaonyesha kilichokuwa kikitukia, jinsi ambavyo ishara na maajabu, na kila kitu, na kile kilichoandikwa.

180 Sasa yeye alisema, “Hawakuingia, kwa sababu ya kutokuamini kwao.” Hawakuamini.

181 “Lakini sasa, sisi, tunaingia katika kipindi cha wakati, basi usiufanye mgumu moyo wako. Usitende kama walivyotenda, katika siku za kukasirisha, wakati walipomkasirisha Mungu.” Walifanyaje jambo hilo? Si kwa kuishi kizinzi. Hebu nisisitize jambo hili kweni.

182 Unasema, “Ndugu Branham, ninaenda kanisani.” Hilo ni sawa. “Sijapata kusema uongo maishani mwangu.” Hilo ni sawa. “Sijawahi kuiba. Sijawahi kufanya *hili, lile*, ama *linginelo*.” Hilo ni zuri sana. Hayo yote ni mazuri. Lakini, hayo yangali siyo dhambi.

183 Dhambi ni wakati Mungu anapojionyesha Mwenyewe nawe unakosa kuliadini jambo Hilo, hutalisikiliza.

184 “Loo,” unasema, “kanisa langu halifundishi jambo Hilo.” Mradi tu Biblia inalifundisha, na Mungu analithibitisha, hilo ndilo sahihi.

Sasa hebu angalia kwa muda kidogo tu. Sasa tutaanza sasa jambo fulani halisi, lenye kilindi sana. Sasa, weka dhamira yako kwenye mfuko wa kizibao chako mpaka utakapotoka nje.

185 Sasa angalia kwa makini sana.

Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya sisi kuingia katika... yake, na tuogope,...

Ya mwanamume, ya mwanamke, viwakilishi nafsi sasa. Ati nini?

...mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.

¹⁸⁶ Sasa, Paulo anajaribu kuwaambia, katika mlango uliotangulia, kuhusu mambo haya yote. Bali sasa anajaribu kuwaambia kwamba ni Nini.

Loo, je! tuna muda? Mimi... Labda afadhali tungojee mpaka usiku wa leo. Wakati unaenda, nasi tutakuwa na ibada ya maombi. Labda afadhali tuendeleo nalo usiku wa leo, sababu hili kweli limejaa vitamini, vitamini za kiroho. Tuna mengi ya kufanya, nami nina kazi nyingi alasiri ya leo. "Hebu tuninii..."

Basi, ikiwa ikaliko ahadi... na tuogope.

¹⁸⁷ Sasa, je! walikuwa na ahadi ya nchi iliyoahidiwa, huko Misri? Na, wakati, Mungu aliposhuka, kuifanya ahadi hii dhahiri. Mbona, Mungu alimwambia Ibrahimu, mamia na mamia ya miaka hapo kabla, ya kwamba atafanya hivyo. Lilikuwa ni la Kimaandiko.

¹⁸⁸ Yusufu alisema, "Msiiondoe mifupa yangu hapa mpaka mtakapokwenda kwenye ile nchi ya ahadi na mnizike huko pamoja na baba zangu wengine." Maana, yeye alijua ufufuo ulikuwa unakuja, hapo Yesu alipofufuka katika wafu, maana alikuwa amejua yale Ayubu aliyosema. Unaona?

¹⁸⁹ Kila mmoja wa hao manabii alijua yale hasa huyo nabii mwingine aliyokuwa amesema, nao walijua ya kwamba Roho wao alikuwa ni mmoja. Nao walikuwa wakingoja. Loo, ndugu! Loo, hilo linapaswa kututikisa kutoka katika hali yetu ya kilimwengu. Walikuwa wameelekeza macho yao, si kwenye yale watu waliyokuwa wakisema, bali yale hao manabii waliyosema. Kila mmoja wao alikuwa akiangalia.

¹⁹⁰ Ibrahimu alisema, "Nizikeni papa hapa ambapo Ayubu alizikwa." Kasema, "Sara, nitanunua kishemu cha ardhi. Tutazikwa papa hapa."

¹⁹¹ Isaka alikuwa ni nabii, kama baba yake. Kasema, "Sikilizeni. Msinizike mahali pengine popote, si hapa Misri, bali nirudisheni moja kwa moja kwenye nchi ya ahadi. Mkanizike papa hapa."

¹⁹² Yakobo alikufa kule kwenye nchi ya ahadi, bali alimwambia mwanawe, aliyekuwa ni nabii, kasema, "Unajua, usiku mmoja Malaika alinigusa ubavuni. Nimechechemea tangu wakati huo. Njoo, weka mkono wangu..." Loo, rehema! "Mwanangu nabii, mimi ni mzee na ni kipofu. Lakini weka mkono wako mtakatifu, kwa kuwa wewe mwenyewe ni nabii, uweke mahali ambapo yule Malaika aliweka mkono Wake, na uniapie kwa Mungu wa Mbinguni ya kwamba hutanzika huku."

193 Na Atukuzwe! Hapo! Je! unaona ufunuo wa kiroho wa Neno? Mbona, nusu ya hao, karibu asilimia tisini, hawakujua yale aliyokuwa akisema. Bali yeye alijua aliyokuwa akisema. “Weka mikono yako ya nabii mahali hapa ambapo Malaika aliweka mkono Wake. Wakati mmoja nilikuwa mwanamume mkubwa, mnene, mwoga, na mwenye nguvu. Lakini, Yeye alinigusa, na tangu wakati huo nimekuwa mtu anayechechemea. Bali nimekuwa mtawala tangu wakati nilipochechemea. Tangu wakati huo nilibadilisha mwenendo wangu, nimekuwa mtawala.” Naam. “Weka mkono wako hapa. Apa kwa Mungu wa Mbinguni, hutanizika hapa.” Kwa nini? Hakuna mtu aliyejua yale aliyokuwa akisema. Yusufu alijua. Alisema, “Nichukueni mnipeleke kule na mkanizike katika ile nchi ya ahadi.” Huko ndiko jambo lilikokuwa. Bila shaka.

194 Wakati Yusufu alipokufa, miaka kadhaa baadaye, yeye alisema, “Msinizike huku. Bali iangalieni mifupa yangu mnapopita, maana siku moja mtaondoka hapa. Na mtakapoondoka, ichukueni mifupa yangu mwende nayo.”

195 Haya basi. Acha ulimwengu useme watakayo, na wafanye wanavyotaka kufanya. Jina la Bwana litukuzwe. Niweke katika Kristo, haidhuru kama nikiitwa kitu chochote... wa siasa kali, mtakatifu anayejifingirisha. Siku moja Yeye yuaja, na wale walio katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye, atakapokuja. Yote ni Kweli ya kiroho iliyofunuliwa iliyolala papo hapo, na inahitaji nia ya kiroho kushika Hilo. Tulieni kwenye hilo, siku nzima. Wazieni jambo hilo. Hata kama hutakula chakula chako cha jioni, wazia jambo hilo.

196 Na usiku wa leo, tutaingia katika Raha Yake, iliyosalia, na tuone kwamba ahadi hii ni kitu gani siku hizi. Kitu hiki ni nini siku hizi? Kama Mungu hana Hiyo hapa katika Biblia, na kuithibitisha, kwamba iko papa hapa sasa, basi mimi ni nabii wa uongo. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini iko hapa. Raha hii ni nini?

197 Yeye alisema:

Sasa, *basi, ikiwa ikaliko ahadi yetu ya kuingia kama tu vile walivyofanya, ... na tuogope.*

198 Nayo inapaswa kuwa ni ahadi ile ile. Inapaswa kuwa ni raha ile ile. Inapaswa kuwa ni Mungu yeye yule. Inapaswa kuwa ni ishara zile zile. Inapaswa kuwa ni jambo lile lile. Bali na tupate raha. Sasa ni Nini? Bwana na atupe hilo, usiku wa leo.

Tunapoinamisha vichwa vyetu.

199 Bwana uhimidiwaye, Umilele pekee ndio utakaofunua hayo mambo makuu ambayo sasa tunayashiriki pamoja. Ni vigumu...

Wapo wengi waliokusudiwa kwenda hukumuni. Kama Wewe ulivyosema katika Kitabu cha Yuda, ya kwamba, “Watu wa kale, waliokusudiwa tangu zamani hukumu, wangeichukuwa neema

ya Mungu wetu na kuibadilisha kuwa ufisadi.” Na wengi siku hizi wanahubiri Injili, neema ya Mungu, wanaifanya kuwa mradi wa kujipatia fedha, wakiwa na kanisa kubwa maarufu na wengi zaidi katika shule ya Jumapili, wakichukua neema ya Mungu na kuibadilisha kuwa ufisadi. Na ulimwengu ni mpofu, na unaenda kama nguruwe wasioona. Hawafahamu.

²⁰⁰ Ee Mungu, tufungulie ufahamu. Jalia ufahamu wetu usiwe kama wa watoto wa ulimwengu huu. Kwa kuwa umesema katika Neno Lako, ya kwamba, “Wana wa ulimwengu huu ni werevu kuliko wana wa Nuru.” Hapo mwanzo ilikuwa hivyo, “watoto wa Kaini” walikuwa ni wanasayansi hodari maarufu. Walikuwa waalimu hodari. Walikuwa wafua vyuma. Waliendelea kufanikiwa, watu wa kidini sana, bali walihukumiwa na kuzamishwa majini katika ile hukumu. Na mizoga yao ilielea majini, na nafsi zao zikaenda kuzimu.

²⁰¹ Na Yesu alienda akazungumza nao, wakati alipokufa. “Na akaenda kuzimu na kuwahubiri nafsi waliokuwa kifungoni, wasiotubu katika uvumilivu, katika siku za Nuhu,” yanasema Maandiko. Na Mungu, wakati aliposimama duniani, alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

²⁰² Lakini tunaona, “ukoo wa Sethi basi,” watu wanyenyekevu, watu halisi wa Mungu, wakiwa hawajui mambo mengi sana ya ulimwengu, wasiojali mambo ya ulimwengu hata kidogo, bali walikuwa wameweka kando kila mzigo na walikuwa wamemwamini Mungu, na wakawa manabii na watu mashuhuri katika ule Ufalme. Wakati hao wengine, ulimwengu huo mwingine wa kidini, waliwacheka, wakawadhihaki. Bali saa iliwadia ambapo mafuriko na hukumu vilikuja.

²⁰³ Ndivyo ilivyokuwa katika kule kuja kwa Yesu Kristo. Jinsi walivyomcheka na kumdhihaki, wakati wakiwa walikuwa na dini zao na makanisa yao makubwa. Bali walimdhihaki Nyota ya Asubuhi, nao wakamcheka. Lakini hata hivyo waliingia hukumuni. Na wakati walipokimbia na kuingia Yerusalemu, huko walikula watoto wao wenyewe, kutokana na njaa kali, na damu yao ikatiririka kwenye malango ya barabara za mji wakati walipoutekeza mji na hekalu, na nafsi zao zikaenda kuzimu.

²⁰⁴ Bwana, sisi hapa tena, kwenye wa tatu. Hiki ni kipindi katika maisha. Tatu ni namba ya nuru. Nasi tumewasili, tukiwa tayari kwa ajili ya Kunyakuliwa.

Kanisa likisonga mbele, ule ulimwengu mkuu wa kisayansi. Makanisa siku hizi yakiwa yamejaa waaminio wenye kushuku. Makumi ya maelfu wakiwa wameandikwa majina yao kwenye kitabu, naam, mamilioni, nao wangeicheka Injili, na kusema, ya kwamba, “Wao hawana elimu. Hawajui.”

Labda hivyo ndivyo ilivyo, Bwana, bali kile tunachopungukiwa katika elimu, Wewe unatufidia katika

neema; kwa kumtuma Malaika Wako wa Nuru, kwa kudhihirisha nguvu Zake, ukithibitisha hayo Maneno kwa wale walio maskini na wajinga kama sisi. Lakini tunakupenda Wewe kwa ajili ya jambo hili, kwa kuwa ni neema ya Mungu iliyofanya jambo hilo, nasi tunajua ya kwamba tulizaliwa. Wala sisi hatupendezi, hata kidogo. Sisi ni wabaya sana. Bali Wewe, kwa neema, ulinyosha mkono Wako wa rehema na umeyafumbua macho yetu, kama vile Yesu alivyotuomba; kama Eliya alivyomwomba Gehazi, alipoangalia aone kilichomzunguka. Na leo macho yetu yamefunguliwa, nasi tunaona mambo ya Mungu, na kujua tunatembea katika wakati wa mwisho; wakati siku za watu wa Mataifa ziko karibu na kwisha, Naye atachukua watu kwa ajili ya Jina Lake. Jalia tuhesabiwe humo, Bwana, tunaomba kwa unyenyekevu. Tunaomba ya kwamba utatujalia hilo.

²⁰⁵ Tubariki. Bariki wasikilizaji hawa wachache asubuhi ya leo. Wametokana na aina mbali mbali za dini na imani, bali waweke kando leo, Mungu. Na jalia waangalie moja kwa moja kuelekea Kalvari, waseme, “Mungu, nifinyange na nitengeneze. Mimi ni kama ninii. . .” Yule nabii alisema ya kwamba alishuka akaenda kwenye nyumba ya mfyanzi, apate kuvunjwa na kufinyangwa upya. Tufinyange na utufananishe na umbo ambalo Mungu angetutaka tuwe. Haidhuru kama itatubidi kuwa jamvi la sakafuni katika Nyumba ya Bwana. Afadhali niwe jamvi la mlangoni kuliko kuishi katika mahema na waovu. Na jalia jambo hilo, Bwana. Tubariki tu sasa, na utudumishe kuwa wanyenyekevu. Jalia mioyo yetu ifunguliwe, nia zetu ziwe safi, kwa mambo ya Mungu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo.

²⁰⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui kama mtu fulani angetaka kukumbukwa katika maombi, kwa ajili ya wokovu wa nafsi yako? Waweza kuinua mkono wako, na ukiwa mwenye dhambi tu? Mungu akubariki wewe, kijana. Mtu mwingine? Mungu akubariki, kule nyuma, bwana. Mungu akubariki, bibi. Mtu mwingine anayetaka kukumbukwa katika maombi sasa hivi, kwa ajili ya nafsi yako? Mungu akubariki, bwana, uliyeinua mkono wako. Na Mungu akubariki, na wewe hapa. Vizuri sana. Kungeweza kuweko na mwingine, kabla tu ya kufunga? Ninajisikia kungekuwako. Mungu akubariki, kule nyuma, bwana, huko nyuma.

²⁰⁷ Aisee, sasa angalia, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sitaki mfikiri hata kidogo ati kwa sababu ni maskani hii ndogo. Sitaki mfikiri ni kwa sababu ni watu hawa. Na Mungu mwenye rehema, msifikiri ni kwa sababu Malaika huyo wa Bwana alipigwa picha pamoja nami, nami. . . na—na kitu kama hicho, kufanya hivyo. Ee Mungu! Kama ningalijisikia hivyo, basi, ndugu, ninapaswa kuwa madhabahuni badala ya kuwauliza ninyi. Lakini ninasema tu jambo hili, ninasema tu jambo hili kwa Maandiko, mpate kuona ya kwamba hii ni Kweli. Kama

ningalilisema jambo Hilo, na hakuna lingine, nikaendelea kama mhubiri mwingine yeyote ama kitu chochote kile, ama yeyote yule, vema, basi, ingekuwa ni jambo la tofauti. Bali unaona jambo hilo, Mungu anarudi moja kwa moja na kuthibitisha jambo hilo kwamba ni Kweli. Unaona? Hilo ndilo linalolifanya kuwa halisi, ni Mungu akilithibitisha. Halafu basi, si hilo tu, bali Neno Lake linasema ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo. Yupo hapa analifanya.

²⁰⁸ Sasa kama wewe huko sawa, moyo wako hauko sawa na Mungu, je! waweza kuinua mkono wako? Useme, “Niombe.” Vema, papo hapo ulipo. Kama mikono minane ama kumi imeinuliwa juu, wakitaka rehema kwa ajili ya nafsi yao. Huku mkiinamisha vichwa vyenu, sasa ombeni. Kumbuka, wewe ndiwe unayepaswa kutubu. Mimi ninakuombea tu, ya kwamba Mungu atakurehemu. Lakini hiyo ndiyo madhabahu, Mungu amewaleta mahali fulani niani mwenu; hiyo ndiyo madhabahu. Tunaamini katika kuja madhabahuni, hakika, lakini hilo halininii—hilo halininii. . . Ni sawa. Bali madhabahu yako halisi ni pale ambapo Mungu amekutana nawe. Naye amekutana nawe papo hapo unapoketi. Hiyo ndiyo madhabahu yako.

²⁰⁹ Sasa sema, “Mungu, nirehemu mimi, mwenye dhambi. Na tangu siku hii na kuendelea, kama utanisaidia, nitakuishia. Nita—nitakutumikia. Sijali mtu yeyote anasema nini, ninatoka, asubuhi ya leo. Ninaombea papa hapa, Nawe niondolee hii roho chafu fidhuli. Niondolee hasira hii. Ninajua siwezi kufanya hivyo na niwe sawa na Mungu. Nami nina chuki moyoni mwangu. Nina wivu. Nina kijicho. Nina *hiki*, *kile*. Kiondoe, Mungu. Sitaki kuwa hivyo. Nifanye mnyofu, na mnyenyekevu, na mpole. Nifanye mwanana. Nifanye mtu ambaye kwamba ningeweza kuwavuta wengine Kwako. Jalia nikufanyie jambo fulani kuonyesha shukrani maishani mwangu.” Hayo ndiyo maombi unayoomba sasa, tunapoomba pamoja.

²¹⁰ Baba wa Mbinguni, hao ni Wako. Hao ni matunda ya Ujumbe asubuhi ya leo. Waliinua mkono wao. Kitu fulani kiliwafanya wafanye hivyo. Wao, waliasi kanuni za uvutano wa dunia walipoinua mikono yao. Kulikuwako na roho ndani yao iliyofanya uamuzi. Waliinua mikono yao, ya kwamba walimkubali Muumba aliyewaumba.

²¹¹ Sasa, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utawabariki, na kuwapa Uzima wa Milele, sasa hivi. Hakuna kitu ningaliweza kufanya; kuwaita madhabahuni, kuwaweka katika chumba kingine, kufanya kazi yote. Hilo, hilo linakuhitaji Wewe kulifanya, Bwana. Sisi hatuwezi kufanya zaidi ya kuhubiri Neno. Wewe ulisema, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno, Neno la Mungu.” Sasa, tumelihubiri Neno, nao wameinua mikono yao, ya kwamba waliliamini. Sasa wape Uzima wa milele, maana Wewe uliahidi utafanya hivyo. Kama walikuwa ni waaminifu katika kuinua mikono yao, watatoka humu jengoni

asubuhi ya leo, Mkristo mnyofu, mpole, mnyenyekevu, kwa maana Wewe uliahidi jambo hilo. Wala Maneno Yako hayawezi kushindwa. Ninaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa ninauangalia, ninaungojea na kuutamani,
Ule Mji unaong'aa, aliouona Yohana ukishuka chini.

Katika Mji ule unaong'aa, (abuduni sasa) Mji mweupe kama lulu,
Nina jumba kubwa, kinubi na taji;
Sasa ninautazamia, ninaungoja na kuutamani,
Ule Mji unaong'aa, aliouona Yohana ukishuka chini.

212 Hivi tu wewe humpendi? Ujumbe umekwisha, sasa. Huku ni kuabudu. Hatuji kanisani kusikia tu ujumbe. Tunakuja kuabudu. Msahau tu mtu aliye karibu yako. Mwabudu Yeye tu. Loo, ni jambo zuri jinsi gani! Ni la ajabu jinsi gani! Mwambie tu kwa niniii yako. . . Si lazima umwambie kwa sauti. Mwambie tu moyoni mwako, "Ninakupenda, Bwana. Nisamehe dhambi yangu." Loo, jamani!

. . . Mji mweupe kama lulu,
Nina jumba, kinubi na taji;
Sasa ninatazamia, ninaungoja na kuutamani,
Ule Mji mweupe, aliouona Yohana ukishuka chini.

213 Baba yetu, Mungu, tupokee. Tunangojea, tunapolisikiliza Neno, tunatamani. "Mioyo yetu inakuonea Wewe kiu, kama ayala anavyokionea kiu kijito cha maji. Nafsi yetu inakuonea kiu Wewe, Ee Mungu." Ninatamani na kungojea, ninaingojea ile saa na wakati Yesu atakapokuja, nikingojea wakati tutakapoitwa mbinguni. Sio kusimama mbele ya Hakimu hukumuni; tayari imepita. Sisi tumekufa kwa mambo ya ulimwengu. Tumeingia ndani ya Kristo, Naye alichukua hukumu yetu. Yeye ni Wakili wetu sasa, kwenye kiti cha haki. Wakili wetu ahimidiwaye, ambaye, tunapokiri, Yeye anatumetea kesi yetu mpaka tunajua ya kwamba hatustahili. Kama maskini dada mmoja asubuhi ya leo, alivyosema katika ushuhuda wake, na akiweka mapeni yake, "Tangu nilipokuja hapa nimejifunza ya kwamba si utakatifu wangu, ni utakatifu wa Mungu."

214 Hakika, Bwana, tunawafundisha watu, hakuna kitu chema katika mwanadamu, hata kimoja. "Mwanadamu ni nini hata umjali?" Bali ni neema ya Mungu iliyotujilia. Nasi tunatumainia tu katika matendo Yake mema, si katika yetu. Nasi tunakuabudu, Mungu Aliye Mtakatifu Sana, kwa ajili ya wema Wako, kutuhesabu katika Ufalme Wako mkuu, katika mipango Yako mikuu. Tunakupokea mioyoni mwetu, kwa imani.

Na kwa neema, tunaamini ya kwamba Wewe umetupa hilo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa utumishi wa Mungu.

²¹⁵ Sasa, Bwana, waponye wagonjwa wanapokuja kuombewa, asubuhi ya leo. Wape hiyo furaha, ambapo wanatamani kuwa wazima. Jalia wajue ya kwamba mateso haya madogo, mepesi, yaliyowekwa juu yao, ni wakati mfupi tu wa kujaribiwa. Mungu anajua yote kuhusu hayo. Aliyafanya hayo ili aone kile tungalifanya kuyahusu. Jinsi ambavyo Mungu... Jalia watoke moja kwa moja wakadai kazi hiyo iliyomalizika! Naomba Wewe... Jalia wasikukasirishe, kwa kukimbia *hapa* na *pale*, na *ndani* na *nje*, “Vema, sijui jambo *hili*, *lile*.”

²¹⁶ Bwana, jalia wachukue msimamo imara, waseme, “Bwana, Wewe Ndiwe uliyeniokoa. Wewe Ndiwe uliyenifanyia mambo haya. Ninakuamini Wewe, Nami ninakutumaini, leo.” Nami naomba ya kwamba utawajalia watu hawa jambo hili, katika Jina la Kristo. Amina.



KITABU CHA WAEBRANIA

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org